NO. 5 OF 1984

# KATIBA YA ZANZIBAR

UTANGULIZI

AZIMIO LA BARAZA LA WAWAKILISHI LA KUWEKA KATIBA YA ZANZIBAR

KATIBA YA ZANZIBAR

1 9 8 4

# KATIBA YA ZANZIBAR

## SURA YA KWANZA

### Zanzibar, Chama na Watu

### Sehemu ya Kwanza

### Zanzibar na Chama

Sehemu:

1. Zanzibar
2. Eneo la Zanzibar na mipaka ya Mikoa, Wilaya n.k.
3. Muhuri wa Serikali na Wimbo.
4. Katiba ya Zanzibar.
5. Chama na mamlaka yake.

Sehemu ya Pili - Watu

6. Mzanzibari
7. Haki ya kupiga kura.

SURA YA PILI

Malengo na Maamuru muhimu ya Sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

8. Wajibu mkubwa wa Serikali
9. Serikali na watu.
10. (1) Malengo ya Kisiasa
    (3) Malengo ya kiuchumi
    (5) Malengo ya jamii.
    (6) Malengo ya kiafya, kielimu na utamaduni.
    (7) Malengo ya kufanya kazi.

SURA YA TATU

Kinga ya Haki za Lazima na Uhuru wa Mtu Binafsi:

11. Usawa wa binaadamu.
12. Usawa mbele ya sheria.
13. Haki ya kuwa hai.

Sehemu:

14. Haki na Uhuru wa mtu binafsi,
15. Haki ya faragha ya mtu na usalama wake.
16. Kinga ya uhuru wa kwenda.
17. Kinga ya kutokana na kudhulumiwa mali.
18. Uhuru wa maoni,
19. Uhuru wa mtu kuamini dini atakayo,
20. Kinga kwa uhuru wa kujikusanya na kujiunga.
21. Uhuru wa kushiriki shughuli za umma, haki ya kufanya kazi na kupata ujira.
22. Wajibu wa kushiriki kazini.
23. Wajibu wa kutii sheria za nchi, kulinda mali ya umma na ulinzi wa Taifa.
24. Mipaka kwa haki na uhuru, na hifadhi kwa haki na wajibu.
25. Haki za lazima na uhuru wa binafsi.

SURA YA NNE

Serikali

Sehemu ya Kwanza

Rais

26. Ofisi ya Rais na sifa za kuchaguliwa kuwa Rais.
27. Uchaguzi wa Rais
28. Muda wa kuendelea na Urais.
29. Kuongezwa kwa kipindi cha miaka 5.
30. Kutofaa kuwa Rais.
31. Kiapo cha Rais.
32. Kuachishwa Urais kwa ugonjwa.
33. Nafasi katika kiti cha Urais.
34. Mpango wa uchaguzi iwapo kiti cha Rais kiwazi.
35. Mshahara na malipo mengine ya Rais.
36. Rais hatashtakiwa akiwa kazini.
37. Hadhi ya Rais aliepita.

Sehemu ya Pili

Waziri Kiongozi

38. Waziri Kiongozi wa Zanzibar.
39. Kuwa wazi kwa Ofisi ya Waziri Kiongozi.

Sehemu:

104. Makadirio.
105. Ruhusa ya matumizi ya mfuko mkuu wa hazina kwa sheria ya matumizi ya fedha.
106. Malipo ni kwa idhini ya hati maalumu.
107. Mfuko wa matumizi ya dharura.
108. Matumizi ya fedha kabla ya sheria kuanza.
109. Deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
110. Malipo ya baadhi ya maafisa.
111. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali.
112. Kumuondoa kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Sehemu ya Pili

Masharti ya fedha yahusuyo Mambo ya Muungano:

Sehemu:

113. Mchango wa Muungano.
114. Uwezo wa kutumia kazma.

SURA YA NANE

Tume ya Utumishi Serikalini:

115. Tume ya Utumishi
116. Uteuzi na kumalizika kwa ujumbe wa mjumbe.
117. Uteuzi wa Wafanyakazi wa Serikalini.

SURA YA TISA

Tume ya Uchaguzi

118. Tume ya uchaguzi
119. Majimbo.

SURA YA KUMI

Idara Maalum

120. Idara Maalum.
121. Tume ya uajiri ya Idara maalum.
122. Uanzishwaji wa Idara Maalum.

Sehemu ya Tatu

Mawaziri, Manaibu Mawaziri na Baraza la Mapinduzi:

40. Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
41. Baraza la Mapinduzi.
42. Ugawaji wa Mawizara kwa Mawaziri.
43. Mikutano ya Baraza.
44. Viapo vya uaminifu.
45. Naibu Mawaziri
46. Nafasi ya Waziri, Memba wa Baraza la Mapinduzi kuwa wazi.
47. Katibu wa Baraza la Mapinduzi.
48. Makatibu Wakuu.

Sehemu ya Nne

Madaraka ya Serikali

49. Madaraka ya Serikali ya Zanzibar.
50. Kutolazimika kwa Rais kufuata ushauri wa mtu
51. Uanzishaji wa Afisi na wadhamini wa Afisi hizo.
52. Muda wa kufanya kazi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.
53. Mwanasheria Mkuu.
54. Kazi za Mwanasheria Mkuu.
55. Kiapo cha uaminifu.
56. Washauri maalum.
57. Uwezo wa kutoa msamaha.
58. Kamati ya ushauri katika uwezo wa kutoa msamaha.
59. Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya.
60. Kazi za Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya.

SURA YA TANO

Baraza la Wawakilishi

Sehemu ya Kwanza

61. Baraza la Kutunga Sheria.
62. Kuanzishwa kwa Baraza la Wawakilishi.
63. Uchaguzi wa Wajumbe wa kuchaguliwa.

Sehemu:

64. Wajumbe wa kuteuliwa.
65. Wajumbe wa kuchaguliwa na Baraza la Wawakilishi
66. Sifa za kuchaguliwa.
67. Kutofaa kuchaguliwa.
68. Kiapo cha Mjumbe Mwakilishi.
69. Tamko rasmi la Wajumbe Wawakilishi kuhusu masharti ya uongozi.
70. Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoa taarifa ya mali.
71. Muda wa wajumbe kushika madaraka yao.
72. Uamuzi wa suala kama mtu ni mjumbe Mwakilishi ama sio.
73. Spika.
74. Naibu Spika.
75. Taratibu za uchaguzi wa Spika na Naibu Spika.
76. Katibu wa Baraza la Wawakilishi.
77. Sekretariet ya Baraza la Wawakilishi.

Sehemu ya Pili
Sheria na Taratibu katika Baraza la Wawakilishi

78. Nguvu ya kufanya sheria.
79. Utaratibu wa Kutunga Sheria.
80. Kubadilisha Katiba.
81. Uongozi wa kikao cha Baraza la Wawakilishi.
82. Viti vilivyo wazi katika Baraza la Wawakilishi na utaratibu wa kuendesha shughuli za Baraza.
83. Upigaji kura katika Baraza la Wawakilishi.
84. Madaraka ya Rais katika Baraza la Wawakilishi.
85. Kamati za Baraza la Wawakilishi.
86. Baraza Kutunga Sheria.
87. Lugha rasmi.
88. Kazi za Baraza la Wawakilishi.

Sehemu ya Tatu
Kuitisha na kuvunja Baraza la Wawakilishi:

89. Kuitisha kikao cha Baraza la Wawakilishi.
90. Uchaguzi Mkuu wa mkutano wa mwanzo.
91. Kusitisha na kuvunja Baraza la Wawakilishi.
92. Maisha ya Baraza la Wawakilishi.

SURA YA SITA
Sheria

Sehemu ya Kwanza

Mahkama Kuu

93. Kuundwa kwa Mahkama Kuu.
94. Uteuzi wa majaji wa Mahkama Kuu.
95. Muda wa kushika madaraka ya ujaji.
96. Viapo kwa majaji wa Mahkama Kuu.

Sehemu ya Pili
Mahkama ya Rufaa.

97. Kutambuliwa kwa Mahkama ya Rufaa.
98. Kazi na uwezo wa Mahkama ya Rufaa.

Sehemu ya Tatu
Mahkama Nyenginezo

99. Kuanzishwa kwa Mahkama nyengine.

Sehemu ya Nne
Utaratibu wa kupeleka Haji na Kutekeleza Maagizo yaliyomo katika Hati zilizotolewa na Mahkama:

100. Utekelezaji wa maagizo ya Mahkama utafanywa nchini Tanzania kote.

Sehemu ya Tano
Tume ya Kuajiri ya Mahkama

101. Tume ya kuajiri ya Mahkama.
102. Uteuzi wa Afisa wa Mahkama.

SURA YA SABA
Fedha

Masharti ya Fedha yahusuyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar:

103. Mfuko Mkuu wa hazina na fedha nyengine za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Sehemu:

104. Makadirio
105. Ruhusa ya matumizi ya mfuko mkuu wa Hazina kwa Sheria ya matumizi ya fedha.
106. Malipo ni kwa idhini ya hati maalumu.
107. Mfuko wa matumizi ya dharura.
108. Matumizi ya fedha kabla ya sheria kuanza.
109. Deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
110. Malipo ya baadhi ya maafisa.
111. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali.
112. Kumuondoa kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Sehemu ya Pili

Masharti ya fedha yahusuyo Mambo ya Muungano:

Sehemu:
113. Mchango wa Muungano.
114. Uwezo wa kutumia kasma.

SURA YA NANE

Tume ya Utumishi Serikalini:

115. Tume ya Utumishi
116. Uteuzi na kumalizika kwa ujumbe wa mjumbe.
117. Uteuzi wa Wafanyakazi wa Serikali.

SURA YA TISA

Tume ya Uchaguzi

118. Tume ya uchaguzi
119. Majimbo.

SURA YA KUMI

Idara Maalum

120. Idara Maalum.
121. Tume ya uajiri ya Idara maalum.
122. Uwezo wa Rais katika Idara Maalum.

SURA YA KUMI NA MOJA

Mamlaka ya baadhi ya Vyombo vya Muungano:

123. Mahkama ya Katiba, Tume ya Kudumu ya Uchunguzi, Tume ya Tabia za Viongozi na Tume ya Uchaguzi Kutumika Zanzibar.

SURA YA KUMI NA MBILI

Vyombo vyengine vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar:

Sehemu ya Kwanza

Baraza la Mipango na Tume ya Kudumu ya Mipango:

124. Baraza la Mipango.
125. Wajumbe wa Baraza
126. Tume ya Kudumu ya Mipango.

Sehemu ya Pili

Serikali za Mitaa

127. Serikali za mitaa.

SURA YA KUMI NA TATU

Mambo ya Jumla

128. Kujiuzulu.
129. Uteuzi mpya na kuarifiwa kwa kuachishwa kazi.
130. Maelezo kuhusu utaratibu wa kukabidhi madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali.
131. Sheria za Muungano.
132. Masharti ya kutoza kodi.
133. Ufafanuzi.
134. Jina la Katiba.

NO. 5 OF 1984

NAKUBALI

Hassan

ALI HASSAN MWINYI
RAIS WA ZANZIBAR
NA
MWENYEKITI WA
BARAZA LA MAPINDUZI
1-12-84

# KATIBA YA ZANZIBAR

## UTANGULIZI

## AZIMIO LA BARAZA LA WAWAKILISHI LA KUWEKA KATIBA YA ZANZIBAR

Kwa kuwa mkutano wa Baraza la Wawakilishi wa tarehe 9 Oktoba, 1984, kwa niaba ya Wananchi wa Zanzibar ulielewa na kukubali kwamba jukumu letu katika historia ya Watu wa Zanzibar ni kuimarisha Umoja, kuendeleza Mapinduzi ya Kijamaa katika Zanzibar na kusukuma Mapambano ya ukombozi na harakati za Mapinduzi nchini, katika Afrika na duniani kote;

KWA KUWA tunatambua kwamba Zanzibar ni jamii ya Watu walio chini ya Serikali moja ya Kidemokrasi yenye lengo maalum la kuweka Utawala wa Sheria;

KWA KUWA tunatambua kwamba Umoja wa Wananchi wa Zanzibar unatokana na ushirikiano wa miaka mingi tangu wakati wa mapambano ya kupigania Uhuru hadi kufikia daraja hii ya mafanikio, na unatokana na siasa yetu ya Ujamaa na Kujitegemea;

KWA KUWA tunazingatia na kuthamini kazi nzuri ya Kimapinduzi iliyofanywa na Viongozi wa Mapinduzi, wakiongozwa na Mwasisi wa Chama cha ASP na Mapinduzi ya Zanzibar ya 1964, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, ambaye fikra zake zitaendelezwa na kudumishwa daima, kizazi baada ya kizazi katika kupambana na Ukoloni, Ubepari, Kiburi, Unyonge, Uonevu na Dharau, na badala yake kudumisha Uhuru na Umoja, Haki na Usawa, Heshima na Utu;

KWA KUWA tunatambua kwamba kuweko kwa Chama cha Mapinduzi kunaongeza upeo wa nguvu na Umoja wetu katika kuendeleza mapambano ya kujenga ujamaa nchini na kushiriki kwa pamoja na kikamilifu katika harakati za Mapinduzi ya Zanzibar, ya Tanzania, ya Afrika na ya Dunia;

KWA KUWA tunatambua kwamba mafundisho na mawazo ya Kimapinduzi yatalindwa, yataendelezwa na kudumishwa kwa misingi ya Kidemokrasi; na

KWA KUWA tunatambua kuwa mapambano ya kujenga Ujamaa katika Zanzibar na kushiriki kwetu kikamilifu katika harakati za Mapinduzi ya Zanzibar kunahitaji SHERIA madhubuti itakayowaongoza watu Ki-Katiba, kutokana na fikra za Wafanyakazi na Wakulima;

NA KWA KUWA SISI, Wananchi wa Zanzibar tumeamua rasmi kwa dhati kujenga katika nchi yetu jamii inayozingatia misingi ya uhuru, haki udugu na amani.

NA KWA KUWA misingi hiyo yaweza tu kutekelezwa katika jamii yenye demokrasi ambayo Serikali yake husimamiwa na Baraza la Wawakilishi lenye wajumbe waliochaguliwa na linalowakilisha wananchi, na pia yenye Mahkama huru zinazotekeleza wajibu wa kutoa haki bila woga wala upendeleo wo wote, na hivyo kuhakikisha kwamba haki zote za binaadamu zinadumishwa na kulindwa, na wajibu wa kila mtu unatekelezwa kwa ukamilifu:

KWA HIYO, BASI KATIBA HII IMETUNGWA NA BARAZA LA WAWAKILISHI KATIKA KIKAO CHAKE CHA TAREHE 9 Oktoba, 1984, kwa niaba ya Wananchi, kwa madhumuni ya kujenga jamii kama hiyo, na pia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Zanzibar inaongozwa na Serikali yenye kufuata misingi ya demokrasi na ya kijamaa.

## SURA YA KWANZA
## ZANZIBAR, CHAMA NA WATU

### Sehemu ya Kwanza

### Zanzibar na Chama

IMETUNGWA NA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

Zanzibar

1. Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Eneo la Zanzibar na mipaka ya Mikoa Wilaya n.k.

2. (1) Eneo la Zanzibar ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba na visiwa vidogo vidogo vilivyovizunguka na bahari yake ambayo kabla ya Muungano ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

(2) Kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Serikali, Rais wa Jamhuri ya Muungano akishauriana na Rais aweza kuigawa Zanzibar katika Mikoa, Wilaya na maeneo mengineyo kwa kufuata utaratibu uliowekwa au kukubaliwa na Chama cha Mapinduzi.

Muhuri wa Serikali na alama nyenginezo.

3. (1) Kutakuwa na Muhuri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao alama yake itakuwa kama itavyokubaliwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi

(2) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakua na uwezo wa kuweka kitu cho chote kitachokua kielelezo cha Serikali kama itavyokubaliwa na Sheria itayotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Katiba ya Zanzibar.

4. Katiba hii ni Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na itakuwa na nguvu za kisheria nchini kote na isipokuwa kutokana na kifungu 80 ikiwa sheria yo yote inatofautiana na Katiba hii, basi katiba hii ndiyo itayokuwa na nguvu na sheria hiyo itakuwa batili kwa kiwango kile ambacho kinahitilafiana.

/2..

Chama na mamlaka yake.

5. (1) Chama cha Mapinduzi (kwa ufupi "CCM") ndicho Chama cha Siasa pekee katika Tanzania na ndicho chenye madaraka ya mwisho katika mambo yote kwa mujibu wa Katiba ya Chama.

(2) Shughuli zote za vyombo vya Umma katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zitaendeshwa chini ya uongozi na usimamizi wa Chama,

(3) Masharti yote yaliyomo katika Katiba hii yatatakiwa yatekelezwe kwa kuzingatia wakati wote madaraka ya Chama kama ilivyoelezwa katika vijifungu (1) na (2) vya kifungu hiki.

## SEHEMU YA PILI

Watu

Mzanzibari

6. Mtu ye yote ambaye ni Mzanzibari kwa mujibu wa sheria iliotungwa na Baraza la Wawakilishi, atawajibika kupata haki zote zinazohusika kwa mujibu wa sheria zilizowekwa.

Haki ya kupiga kura.

7.(1) Mzanzibari ye yote aliyetimia umri wa miaka 18 na ambaye hakuzuiliwa na sheria yo yote ile kupiga kura, atakuwa na haki ya kupiga kura katika uchaguzi wo wote ule uliopo Zanzibar,

(2) Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga Sheria inayohusu uchaguzi wa Rais Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani wa Serikali za Mitaa.

(3) Bunge la Jamhuri ya Muungano linaweza kutunga sheria inayohusu uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Wabunge na Sheria hiyo itatumika Zanzibar kwa kulingana na masharti ya kifungu cha 131 cha Katiba hii.

/3..

## SURA YA PILI

### Malengo na Maamuru Muhimu ya Sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Wajibu Mkubwa wa Serikali

8. Itakuwa ni wajibu wa vyombo vyote vya Serikali pamoja na vyombo vyengine vyenye uwezo pamoja na watu wenye kutunga sheria kutawala au uwezo wa kimahkama kufuata misingi ya siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

Serikali na Watu

9.(1) Zanzibar itakuwa ni nchi ya Ujamaa na Kujitegemea yenye misingi ya kidemokrasi na haki za Kijamii.

(2) Kwa hivyo hapa inaelezwa rasmi kwamba:-

(a) Mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa Serikali kufuatana na Katiba utatoka kwa wananchi wenyewe;

(b) usalama na hali nzuri kwa wananchi itakuwa ndiyo lengo kubwa la Serikali;

(c) Katiba hii itahakikisha kwamba wananchi wanashiriki katika Serikali yao.

(3) Muundo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na utendaji wa kazi zake utafanywa katika utaratibu utakaohakikisha kuendelezwa kwa umoja nchini na lengo la kufikia Ujamaa na Kujitegemea.

Malengo ya kisiasa.

10. Kwa madhumuni ya kuendeleza umoja katika nchi itakuwa ni wajibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar:-

(1) kutoa huduma za kutosha kwa ajili ya kuendeleza watu katika njia za mtu kuwa huru kwenda atakapo na utoaji huduma kwa watu wote na kutoa haki zote za kuishi kwa Mzanzibari sehemu zote za Zanzibar;

(2) Kuondosha kabisa vitendo vya rushwa na utumiaji mbaya wa cheo.

Malengo ya Kiuchumi.

(3) Itadhibiti uchumi wa nchi kufuatana na misingi na madhumuni yaliyoelezwa na Katiba hii, na kwa mujibu wa sera za Chama; itadhibiti uchumi wa nchi katika utaratibu utakaohakikisha huduma bora kabisa, na itadhibiti na kuendesha sekta muhimu za uchumi.

(4) Itatoa mwongozo wake katika Katiba kuhakikisha maendeleo ya uchumi yenye urari na yaliyopangika na kwamba mfumo wa kiuchumi hautafanyika katika utaratibu utakaopelekea kulimbikiza kwa utajiri na njia za kuzalisha mali kwa watu wachache au kikundi fulani.

Malengo ya jamii.

(5) Katika kutekeleza siasa hiyo, kuhakikisha kwamba kila Raia atakuwa na haki sawa, majukumu na fursa sawa kwa mujibu wa sheria, utu wa mtu utaheshimiwa na heshima ya mtu itaenziwa na kuendelezwa na kwamba uhuru, kutopendelea na uaminifu wa Mahkama pamoja na kupata fursa kwa urahisi ya kwenda katika Mahakama hizo kutapatikana na kuheshimiwa.

Malengo ya kiafya, kielimu na Utamaduni.

(6) Italenga Siasa yake katika kuhakikisha kwamba zipo huduma za kutosha za kiafya kwa watu wote, zipo fursa sawa na za kutosha za kielimu katika madaraka yote na kwamba utamaduni wa Zanzibar unalindwa, unaimarishwa na unaendelezwa.

Malengo ya kufanya kazi.

(7) Kwamba kila mtu mwenye uwezo wa kufanyakazi anafanya kazi, na kazi maana yake ni shughuli ye yote ya halali inayompatia mtu riziki yake, na kwamba msaada unatolewa kwa wale wasiojiweza wazee, wagonjwa, watoto na walemavu.

## SURA TATU

### Kinga ya Haki za Lazima na Uhuru wa Mtu Binafsi

Usawa wa binaadamu.

11. (1) Binaadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa.

(2) Kila mtu anastahiki heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.

Usawa mbele ya sheria.

12. (1) Watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki, bila ya ubaguzi wo wote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.

(2) Hakuna sheria itakayokuwa na kifungu cho chote ambacho ni cha ubaguzi wa moja kwa moja au kwa taathira yake.

(3) Haki za raia, wajibu na masilahi ya kila mtu yatalindwa na kuamuliwa na mahakama pamoja na vyombo vya nchi na vinginevyo vilivyowekwa na sheria.

(4) Hakuna mtu atakayebaguliwa na mtu ye yote anayefanya kazi chini ya sheria yo yote au katika utekelezaji wa kazi ya ofisi yo yote ya Serikali au uongozi mwengine wa Chama na vyombo vyake.

(5) Katika kifungu hiki neno "kubagua" maana yake ni kutimiza haja kwa watu mbali mbali kwa kutegemea utaifa wao, kabila, pahala walipotokea, muelekeo wake kisiasa, rangi au dini ambapo watu wa aina fulani wanaonekana kuwa ni dhaifu na duni au kuwekwa vikwazo na vipingamizi ambavyo wale watu wa aina nyengine hawawekeani au wanapewa fursa au faida ambayo hawapewi watu wa aina nyengine.

(6) Kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria Serikali itaweka taratibu zinafofaa na zitakazozingatia misingi kwamba:-

(a) wakati haki na wajibu wa mtu ye yote vinahitaji kufanyiwa uamuzi wa mahakama au chombo kinginecho kinachohusika basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa na pia haki ya kukata rufaani au ya kupata kitulizo kinginecho cha kisheria kutokana na maamuzi ya mahakama au chombo hicho kinginecho kinachohusika.

/6..

(b) mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai hatachukuliwa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo; na

(c) ni marufuku kwa mtu kuadhibiwa kwa sababu ya kitendo cho chote ambacho alipokitenda hakikuwa ni kosa chini ya sheria, na pia itakuwa ni marufuku kwa adhabu kutolewa ambayo ni kubwa kuliko adhabu iliyokuwepo wakati kosa linalohusika lilipotendwa;

(d) Kwa ajili ya kuhifadhi haki ya usawa wa binaadamu katika shughuli zote zinazohusu upelelezi na uendeshaji wa mambo ya jinai, katika shughuli nyinginezo ambapo mtu anakuwa chini ya ulinzi bila ya uhuru, na katika kuhakikisha utekelezaji wa adhabu, heshima ya utu wa mtu itatunzwa.

Haki ya kuwa hai.

13. (1) Kila mtu anayo haki ya kuwa na hifadhi ya maisha yake.

(2) Kila mtu anayo haki ya kuishi, na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria.

Haki ya uhuru wa mtu binafsi.

14. (1) Kila mtu anayo haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru.

(2) Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na kuishi kwa uhuru, itakuwa ni marufuku kwa mtu ye yote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vinginevyo isipokuwa tu:-

(a) katika hali na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria; au

(b) katika kutekeleza hukumu, amri au adhabu iliyotolewa na mahkama kutokana na shauri au na kosa la jinai ambalo mtu amekutwa na hatia ya kulitenda.

/7..

Haki ya faragha ya mtu na usalama wake.

15.(1) Kila mtu anastahiki kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafasi yake; maisha yake binafsi na ya nyumbani kwake, na pia heshima na hifadhi ya maskani na mawasiliano yake.

(2) Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kwa mujibu wa kifungu hiki, Mamlaka ya Nchi itaweka utaratibu wa sheria kuhusu hali, namna ya kiasi ambacho haki ya mtu na faragha na ya usalama wa nafsi yake, mali yake na maskani yake, yaweza kuingiliwa bila ya kuathiri kifungu hiki nha Katiba hii.

Kinga ya uhuru wa kwenda

16.(1) Hakuna mtu atakayenyimwa uhuru wake wa kwenda, na kwa madhumuni ya kifungu hiki uhuru uliotajwa humu maana yake ni haki ya kwenda popote katika Zanzibar, haki ya kuishi katika sehemu yo yote ya Zanzibar, haki ya kuingia Zanzibar, haki ya kuondoka Zanzibar na kinga ya kutofukuzwa Zanzibar.

(2) Kizuizi cha kutokutembea kwa mtu ye yote kutokana na kuwekwa ndani kwake kisheria, haitochukuliwa kuwa inapinga au ni kinyume na kifungu hiki.

Kinga kutokana na kudhulumiwa mali.

17. Hakuna mali ya mtu ye yote itayochukuliwa kwa nguvu na hakuna riba au haki yo yote inayotokana na mali hiyo itayochukuliwa kwa nguvu isipokuwa pale ambapo masharti yafuatayo yametimizwa, yaani:-

(a) kumilikiwa au kuchukuliwa kwa mali hiyo ni muhimu sana kwa ajili ya ulinzi, usalama wa wananchi, mazingira ya afya, kuimarisha maendeleo ya upangaji wa mji pamoja na kuendeleza mambo ambayo yataleta faida kwa wananchi kwa ujumla;

(b) umuhimu wa kuchukuliwa kitu hicho ni mkubwa sana hata kwamba unahalalisha uchukuaji wake hata kama utampa ugumu na matatizo mwenye mali hiyo; na

(c) sheria imewekwa kuhusiana na umilikaji au uchukuaji huo kwa kutoa fidia inayolingana.

Uhuru wa maoni.

18. (1) Bila ya kuathiri sheria za nchi, kila mtu yuko huru kuwa na maoni yo yote na kutoa nje mawazo yake, na kutafuta kupokea na kutoa habari na dhana kupitia chombo cho chote, bila ya kujali mipaka ya nchi, na pia ana uhuru wa mawasiliano yake kutoingiliwa kati.

(2) Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbali mbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi, na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii.

Uhuru wa mtu kuamini dini atakayo.

19. (1) Kila mtu anastahili kuwa na uhuru wa mawazo, wa imani na wa uchaguzi katika mambo ya dini, pamoja na uhuru wa kubadilisha dini au imani yake.

(2) Bila ya kuathiri sheria zinazohusika za Jamhuri ya Muungano, kazi ya kutangaza dini, kufanya Ibada na kueneza dini itakuwa huru na jambo la hiari ya mtu binafsi; na shughuli na uendeshaji wa jumuiya za dini zitakuwa nje ya shughuli za Mamlaka ya Nchi.

(3) Kila palipotajwa neno "dini" katika kifungu hiki ifahamike kwamba maana yake ni pamoja na madhehebu ya dini, na maneno mengineyo yanayofanana au kuambatana na neno hilo nayo yatatafsiriwa kwa maana hiyo.

Kinga kwa uhuru wa kujikusanya na kujiunga.

20.(1) Isipokuwa kwa hiari yake, hakuna mtu atakayezuiwa kufurahia uhuru wake wa kuchanganyika au kujiunga, yaani haki yake ya kuchanganyika na kujihusisha atakavyo na watu wengine na hasa kuunda au kuwa mwanachama wa vyama vya wafanyakazi au vyama vyengine kwa faida yake na ambavyo vimekubaliwa kisheria.

(2) Hakuna chochote kilichomo ndani ya au kufanywa chini ya sheria yo yote kitakachohesabiwa kuwa hakilingani au ni kinyume na kifungu hiki (katika kiwango ambacho sheria mama inaeleza):-

(a) mambo yanayotakiwa kwa faida ya ulinzi, usalama wa raia, mazingara ya afya na jamii;

(b) mambo yanayotakiwa kwa madhumuni ya kulinda haki na uhuru wa watu wengine;

(c) mambo yanayotakiwa kuweka makatazo fulani kwa maofisa wa Serikali, Wanajeshi au watu wanaofanya kazi chini ya Serikali za mitaa;

Uhuru wa kushiriki shughuli za umma, haki ya kufanya kazi na kupata ujira.

21. (1) Kila Mzanzibari anayo haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi waliochaguliwa kwa hiari.

(2) Kila Mzanzibari anayo haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye; maisha yake au yanayolihusu Taifa.

(3) Kila Mzanzibari anayo haki ya kufanya kazi na anastahili fursa na haki sawa, kwa masharti ya usawa, ya kushika nafasi yo yote ya kazi na shughuli yo yote iliyoko chini ya Mamlaka ya Zanzibar.

(4) Kila mtu, bila ya kuwapo ubaguzi wa aina yo yote, anayo haki ya kupata ujira unaolingana na kazi yake na, watu wote wafanyao kazi kulingana na uwezo wao watapata malipo kulingana na kiasi na sifa za kazi wanayoifanya.

Wajibu wa kushiriki kazini.

22.(1) Kazi pekee ndiyo huzaa utajiri wa mali katika jamii, ndilo chimbuko la ustawi wa wananchi na kipimo cha utu, kila mtu anao wajibu wa:-

(a) Kushiriki kwa kujituma na kwa uaminifu katika kazi halali na ya uzalishaji mali; na

(b) kutimiza nidhamu ya kazi na kujitahidi kufikia malengo ya uzalishaji ya binafsi na ya pamoja yanayotakiwa au yaliyowekwa na sheria.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha kwanza (1), hakutakuwepo na kazi ya shuruti katika Zanzibar.

Wajibu wa kutii sheria nchi, kulinda mali na ulinzi wa Taifa.

23.(1) Kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii Katiba hii na sheria za Zanzibar, kuchukua hatua za kisheria kama zilivyowekwa, kuhakikisha hifadhi ya Katiba na sheria za nchi.

(2) Kila mtu ana wajibu wa kulinda maliasili ya Zanzibar, mali ya Nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi, na pia kuiheshimu mali ya mtu mwingine.

(3) Watu wote watatakiwa na sheria kulinda vizuri mali ya Zanzibar na kwa pamoja kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu na kuendesha uchumi wa Zanzibar kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadae ya Taifa lao.

(4) Kila Mzanzibar ana wajibu wa kulinda, kuhifadhi na kudumisha uhuru, mamlaka, ardhi na umoja wa Zanzibar.

(5) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga sheria zinazofaa kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kutumikia katika majeshi na katika ulinzi wa Taifa.

Mipaka kwa haki na Uhuru, na hifadhi kwa haki na wajibu.

24.(1) Haki na uhuru wa binaadamu ambavyo misingi yake imeorodheshwa na Katiba hii havitatumiwa na mtu mmoja kwa namna ambayo itasababisha kuingiliwa kati au kukatizwa kwa haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma.

(2) Ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika sehemu hii ya Sura hii ya Katiba hii, yanayofafanua misingi ya haki, uhuru na wajibu wa binaadamu, hayabatilishi sheria yo yote iliyotungwa wala kuzuia sheria yo yote kutungwa au jambo lo lote halali kufanywa kwa mujibu wa sheria hiyo kwa ajili ya:-

(a) kuhakikisha kwamba haki na uhuru wa watu wengine au masilahi ya umma haviathiriwi vibaya na matumizi ya uhuru na haki za watu binafsi;

(b) kuhakikisha ulinzi, usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii, afya ya jamii, mipango ya maendeleo ya miji na vijiji, ukuzaji na matumizi ya madini, au ukuzaji na uendelezaji wa mali au maslahi nyinginezo zo zote kwa njia za kukuza manufaa ya umma;

(c) kuhakikisha utekelezaji wa hukumu au amri ya mahkama iliyotolewa katika shauri lo lote la madai au la jinai;

(d) kulinda sifa, haki na uhuru wa watu wengine au maisha binafsi ya watu wanaohusika katika mashauri mahakamani; kuzuia kutoa habari zinazopatikana kwa siri; kutunza heshima, mamlaka na uhuru wa mahakama;

(e) kuweka vizuizi, kusimamia na kudhibiti uanzishaji, uendeshaji na shughuli za vyama na mashirika ya watu binafsi nchini; au

(f) kutaifishwa mali yo yote kufuatana na maagizo ya hukumu au amri ya mahakama, au kwa lazima kwa manufaa ya umma, na

(g) kuwezesha jambo jingine lo lote kufanyika ambalo linastawisha au kuhifadhi masilahi ya Taifa kwa jumla.

(3) Mtu ye yote anayedai kuwa sharti lo lote katika sehemu hii ya Sura hii au katika sheria ye yote inayohusu haki yake au wajibu wake, limevunjwa, linavunjwa au inaelekea litavunjwa na mtu ye yote Zanzibar, anaweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu.

(4) Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyomo katika Katiba hii Mahakama Kuu itakuwa na mamlaka ya kusikiliza kwa mara ya kwanza shauri lo lote lililoletwa mbele yake kwa kufuata kifungu hiki; na Mamlaka ya Nchi yaweza kuweka sheria kwa ajili ya:-

(a) kusimamia utaratibu wa kufungua mashauri kwa mujibu wa kifungu hiki,

(b) kufafanua uwezo wa Mahakama Kuu katika kusikiliza mashauri yaliyofunguliwa chini ya kifungu hiki;

(c) kuhakikisha utekelezaji bora wa madaraka ya Mahakama Kuu, hifadhi na kutilia nguvu haki, uhuru na wajibu kwa mujibu wa Katiba hii.

(5) Mbali na masharti ya kifungu cha 24 (2) cha Katiba hii sheria yo yote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi haitakuwa batili kwa sababu tu kwamba inawezesha hatua kuchukuliwa wakati wa hali ya hatari, au wakati wa hali ya kawaida kwa watu wanaoaminika kuwa wanafanya vitendo vinavyohatarisha au kudhuru usalama wa Zanzibar ambavyo vinakiuka masharti ya kifungu cha 13 na 14 cha Katiba hii:

Haki za lazima na uhuru wa binafsi.

25. Ilivyokuwa kila mtu wa Zanzibar anawajibika kupata haki zake za lazima na uhuru wa kibinafsi bila, ya kujali kabila, pahala alipotokea au maskani au mahusiano mengine yo yote yale, mtazamo wa kisiasa alionao, rangi, dini au jinsi, lakini mradi iwe uhuru wake unaheshimu haki na uhuru wa wengine na iwe kwa faida ya jamii, basi atakuwa na haki kupata haki kwa kila kimoja na kwa vyote vya hivi vifuatavyo:-

(a) maisha yake, uhuru wake, usalama wake na kulindwa na sheria;

(b) uhuru wa kufikiri, wa kujieleza, wa mkusanyiko na mchanganyiko; na

(c) haki ya kuweza kukaa faragha katika nyumba yake na kulindwa kwa mali yake pamoja na kutokuchukuliwa mali hiyo bila kupewa fidia ipasavyo;

maelezo ya Sura hii yatakuwa na madhumuni ya **kuwezesha** kulinda haki hizo na uhuru kulingana na mipaka maalum ya haki hizo na uhuru kama ilivyoelezwa katika vifungu vinavyohusika kwa mipaka iliyowekwa ili kuhakikisha kwamba kutumika kwa haki hizo na uhuru huo wa mtu binafsi hakuathiri haki na uhuru wa wengine au maslahi ya Taifa kwa ujumla.

SURA YA NNE

Serikali

Sehemu ya Kwanza

Rais

Ofisi ya Rais na Sifa za Kuchaguliwa kwa Rais.

26. (1) Kutakuwa na Rais wa Zanzibar ambaye ndiye atakaekuwa Kiongozi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

(2) Mtu ye yote anaweza kufaa kuchaguliwa kuwa Rais ikiwa:-

(a) ni Mzanzibari,
(b) ameshatimia umri wa miaka 40 na
(c) anazo sifa za kumuwezesha kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Uchaguzi wa Rais.

27. (1) Rais atachaguliwa kufuatana na Katiba hii na kwa mujibu wa sheria yo yote itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi kuhusu uchaguzi wa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

(2) Uchaguzi wa Rais utafanyika katika tarehe itakayowekwa na Tume ya Uchaguzi.

(3) Uchaguzi wa Rais utafanyika si chini ya siku sitini na si zaidi ya siku thalathini kabla ya kwisha muda wa Rais aliyetangulia.

(4) Kwa madhumuni ya uchaguzi huo, Zanzibar itahesabika kuwa ni jimbo moja.

Mtu yeyote aliyejiandikisha kupiga kura katika kumchagua mjumbe wa Baraza la Wawakilishi atakuwa na uwezo wa kupiga kura katika uchaguzi wa Rais.

Muda wa kuendelea na Urais.

28. (1) Kufuatana na Katiba hii mtu ataendelea kuwa Rais mpaka:-

(a) Rais anayefuata ale kiapo cha kuwa Rais;
(b) afariki wakati akiwa Rais;
(c) hapo atapojiuzulu na kukubalika;
(d) iwapo amechaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
(e) pale Baraza la Wawakilishi linapovunjwa; au
(f) kwa sababu ye yote nyengine amewacha kuwa Kiongozi kwa mujibu wa vifungu vyengine vya Katiba hii.

(2) Kufuatana na maelezo ya kijifungu (1) cha kifungu hiki, Rais ataacha madaraka yake baada ya kumalizika miaka mitano kuanzia tarehe ambapo:-

(a) kama yeye ni mtu ambaye ndio mara ya kwanza kuchaguliwa kuwa Rais chini ya Katiba hii alipokula kiapo cha uaminifu na kiapo cha kuwa Rais na

/15..

(b) kwa sababu nyenginezo mtu wa mwisho kushika madaraka hayo kwa mujibu wa Katiba hii alipokula kiapo cha uaminifu na kiapo cha kuwa Rais, au pasingelikuwa na sababu ya kifo chake, basi angalikula kiapo hicho.

(3) Bila ya kuathiri cho chote kilichomo katika kifungu hiki cha Katiba hii hakutakua na mtu ye yote ataechaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar kwa zaidi ya vipindi viwili mfululizo vya miaka mitano kila kimoja.

Kuongezwa kwa kipindi cha miaka 5.

29. Ikiwa Tanzania imo katika vita ambapo Zanzibar pia inahusika na ikiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anaona kuwa ni muhimu kuzuia uchaguzi, Baraza la Wawakilishi, linaweza kwa kupitisha azimio, kuzidisha muda wa miaka 5 iliotajwa kwenye kijifungu cha (2) cha kifungu 28 katika kipindi hadi kipindi lakini hakutakuwa na kipindi kitakachozidi miezi sita mfululizo.

Kutofaa kuwa Rais.

30. (1) Mtu hatofaa kuchaguliwa kuwa Rais ikiwa:

(a) amefanya kitendo chochote, au hitilafu yoyote ambapo kama angekuwa ni mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kungemfanya asite kuwa Mjumbe wa Baraza hilo.

(b) amechaguliwa kushika madaraka hayo katika vipindi viwili mfululizo vilivyokwisha. isipokuwa kwamba kijifungu hiki kisitafsirike kuwa inamzuia mtu huyo kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Katika muda wake wa Urais, Rais hatashika madaraka yo yote mengine yenye mapato isipokuwa yale ya Urais.

Kiapo cha Rais.

31. (1) Mtu anayechukua madaraka ya Urais, kabla ya kuanza wadhifa huo, atakula kiapo cha uaminifu na kiapo cha kazi kama kitavyowekwa na Baraza la Wawakilishi lakini kwa hali yo yote itabidi ashike madaraka hayo kabla ya kupita siku saba baada ya kuchaguliwa.

(2) Viapo hivyo vilivyotajwa vitaendeshwa na Jaji Mkuu wa Zanzibar au iwapo hayupo, vitaendeshwa na mtu anayeshikilia nafasi hiyo.

Kuachishwa Urais kwa ugonjwa.

32. (1) Suala lo lote la kwamba Rais au mtu ye yote anayefanya kazi au kutaka kufanya kazi za Rais, hawezi kwa sababu ya maradhi ya kimwili au kiakili, itaamuliwa kwa mujibu wa kifungu hiki.

(2) Iwapo suala ni kwamba Rais hawezi kufanya kazi zake kwa maradhi ya kimwili au kiakili na ikiwa Jaji Mkuu ameombwa na Baraza la Mapinduzi, kulishughulikia suala hilo, hapo:-

(a) Jaji Mkuu atateua Kamati ambayo itakuwa na watu si chini ya watano ambao kati yao ni madaktari, na watu wawili wanaofaa kuwa Majaji wa Mahkama Kuu.

(b) Kamati hiyo itafanya utafiti kuhusiana na hali ya Rais na baadaye itapeleka ripoti yake kwa Jaji Mkuu ikieleza maoni yake iwapo Rais huyo kwa maradhi aliyonayo ya kimwili au akili, kama hawezi kufanya kazi za Urais; na

(c) Jaji Mkuu atathibitisha kwa kadri aonavyo na atapeleka hati ya uthibitisho kwamba Rais hawezi kufanya kazi zake kutokana na maradhi ya kimwili au kiakili mbele ya Halmashauri Kuu ya Taifa kwa kupata idhini yake au kukataa.

(3) Hati ya Jaji Mkuu chini ya kifungu hiki itakuwa na nguvu za mwisho kwa mujibu wa Katiba hii na haitotiliwa shaka na mahkama yo yote.

Nafasi katika kiti cha Urais.

33. (1) Iwapo **kiti** cha Urais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kiwazi:-

(a) kwa sababu ya kufariki; au
(b) kwa sababu ya kujiuzulu kwa Rais huyo; au
(c) kwa sababu ya maradhi.

watu wafuatao, kwa mujibu wa mpangilio, watashika nafasi hiyo:-

(i) Waziri Kiongozi, au ikiwa hayupo;
(ii) Spika wa Baraza la Wawakilishi na yeye akiwa hayupo;
(iii) Jaji Mkuu wa Zanzibar.

(2) Iwapo kiti cha Urais

(a) kwa sababu Rais anataka kuondoka Tanzania au
(b) kwa sababu nyengine yo yote ile Rais anaweza kwa maandishi na kufuatana na masharti atakayoainisha akayatoa madaraka yake kwa mujibu wa mpangilio, kwa:-

(i) Waziri Kiongozi au naye ikiwa hayupo;
(ii) Mjumbe mmoja wa Baraza la Mapinduzi ambae ni Waziri na ambae ana uzoefu mkubwa katika shughuli hizo kulingana na wengine.

(3) Iwapo mtu ye yote anafanya shughuli za Rais chini ya vijifungu (1) na (2) vya kifungu hichi, ataendelea kufanya shughuli hizo mpaka atapo rejea mmoja kati ya watu waliomtangulia katika kijifungu cha (1) cha kifungu hichi mpaka hapo atakapochaguliwa Rais mwengine, au kwa shughuli za kijifungu cha (2) hadi hapo Rais ataporejea nchini au atapobatilisha uwezo huo alionao.

Mpango wa Uchaguzi iwapo kiti cha Rais kiwazi.

34. (1) Endapo kiti cha Rais **kiwazi** kwa sababu ya au kujiuzulu au kwa maradhi chini ya kifungu cha 33 cha Katiba hii, uchaguzi wa Rais utafanyika katika kipindi cha siku tisiini mara baada ya kiti hicho kuwa wazi na utaendeshwa kwa utaratibu ulioelezwa na kijifungu (2) cha kifungu hiki.

(2) Itakapotokea haja ya kufanyika uchaguzi wa Rais chini ya kijifungu (1) cha kifungu hiki Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama iliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Chama cha Mapinduzi 1982, itakutana na kupendekeza si chini ya majina ya watu wawili walio wa Zanzibari waliofikia umri usio chini ya miaka 40 na ambao wana sifa za kusimama kwenye uchaguzi wa Rais,

(b) majina hayo ya watu waliopendekezwa na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama kwa mujibu wa maelezo ya kijifungu (a) cha kijifungu hiki yatapelekwa kwenye Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama ambayo baadaye itakutana na kumteua mtu mmoja ambaye atakuwa mgombea pekee katika uchaguzi wa Rais kwa mujibu wa maelezo ya kifungu hiki;

(c) Pale Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama itakapothibitisha uteuzi wa mtu ambaye jina lake limeletwa mbele yake, mtu huyo atasimama kwenye uchaguzi na watu wanaweza kumpigia kura ama kumkubali au kumkataa, na endapo katika matokeo ya uchaguzi huo:-

(i) Zaidi ya asilimia hamsini zimemkubali, mtu huyo atachaguliwa kuwa Rais na Tume ya Uchaguzi itatangaza hivyo.

(ii) Kura nyingi zilizopigwa hazikumkubali mtu huyo hatachaguliwa kuwa Rais na inapotokea hivyo Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa itakutana tena na kupendekeza majina ya watu wengine walio wa Zanzibari ambao wametimia umri wa miaka isiopungua arubaini, na baadae Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama pia itakutana tena na kuteua jina la mtu mwengine katika utaratibu ulioelezwa na kijifungu (b) cha kijifungu hiki na baadae utafanyika upigaji mwengine wa kura kwa mujibu wa kijifungu hiki.

Mshahara na malipo mengine ya Rais.

35. (1) Rais atapokea mshahara na posho, na anapostaafu atapata malipo ya uzeeni, kiinua mgongo au posho, kama itakavyoamuliwa na Baraza la Wawakilishi.

(2) Mshahara na posho la Rais hautopunguzwa wakati akiwa bado ni Rais.

(3) Pesa zote zilizoainishwa na kifungu hiki zitatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina.

Rais hatashtakiwa akiwa kazini.

36. (1) Hakuna mashtaka yo yote ya jinai yatakayofunguliwa au kuendelezwa dhidi ya Rais wakati akiwa kazini, au dhidi ya mtu ye yote ambaye anafanya kazi ya Urais kwa mujibu wa kifungu cha 33 cha Katiba hii.

(2) Hakuna mashtaka ya kuhukukia ambapo kuna madai kuhusiana na kitu cho chote kilichotendwa au kuachwa kutendwa yatakayoanzishwa na kuendelezwa dhidi ya Rais wakati akiwa kazini, au dhidi ya ye yote anayefanya kazi za Urais.

(3) Iwapo kuna sheria imewekwa ambayo inaweka muda maalum ambapo mashtaka ya aina yo yote yanaweza kuanzishwa dhidi ya mtu ye yote muda wote ambapo mtu anakuwa Rais au kufanyakazi za Rais hautahesabiwa kuwa ni muda maalum kuhusiana na sheria hiyo iwapo mashtaka yo yote ya aina kama yaliyotajwa katika kijifungu (1) au (2) ni dhidi ya mtu huyo.

Hadhi ya Rais aliepita.

37. Itakua ni jukumu la Serikali kulinda hadhi ya mtu ye yote atakae acha kiti cha Urais kwa sababu ya kutochaguliwa tena, muda wake kumalizika, kujiuzulu au kwa sababu nyengine yo yote iliyo chini ya misingi ya Katiba hii kama itavyokubaliwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

/20..

Sehemu ya Pili
Waziri Kiongozi

Waziri Kiongozi wa Zanzibar.

38. (1) Kutakuwa na Waziri Kiongozi wa Zanzibar ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Rais atamteua Waziri Kiongozi kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuzingatia kwamba hakuna uteuzi wa Waziri Kiongozi utakaofanyika katika wakati wo wote ambapo kazi za Rais zinafanywa na mtu mwengine zaidi ya yeye mwenyewe.

(3) Waziri Kiongozi atakuwa ndiye Mshauri Mkuu wa Rais katika utekelezaji wa kazi zake na pia atakuwa na madaraka juu ya udhibiti, usimamizi na utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na pia atakuwa Kiongozi wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi.

(4) Waziri Kiongozi hatoanza kazi zake mpaka ale kiapo cha uaminifu na kiapo chengine katika utendaji wa kazi zake kama kitakavyowekwa na Baraza la Wawakilishi.

Kuwa wazi kwa ofisi ya Waziri Kiongozi.

39. (1) Endapo nafasi ya Waziri Kiongozi iwazi:-

(a) kwa sababu ya kufariki au kujiuzulu;

(b) ikiwa Rais ameamuru hivyo;

(c) ikiwa mshika wadhifa huo ameacha kuwa ni mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu nyengine zaidi ya kuvunjwa kwa Baraza hilo.

(d) mara kabla ya Rais mpya hajashika madaraka;

Rais atamteua Waziri Kiongozi.

(2) Endapo Waziri Kiongozi anakusudia kuondoka Tanzania anaweza kwa kushauriana na Rais na kwa kufuatana na masharti maalum atakayoweka kwa maandishi kumchagua Waziri ye yote, kufuatana na uzoefu wake, kufanyakazi za Waziri Kiongozi.

Sehemu ya Tatu

Mawaziri, Naibu Mawaziri na Baraza la Mapinduzi

Wizara za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

40. (1) Kutakuwa na Wizara za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama zitakavyoanzishwa na Rais.

(2) Rais kwa kushauriana na Waziri Kiongozi atateua Mawaziri kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Isipokuwa tu, kama ipo haja ya uteuzi wa Waziri yo yote katika kipindi ambacho Baraza la Wawakilishi limevunjwa, mtu ambaye alikuwa ni mjumbe wa Baraza hilo mara kabla ya kuvunjwa anaweza kuchaguliwa kushika wadhifa huo.

Baraza la Mapinduzi.

41. (1) Kutakuwa na Baraza la Mapinduzi ambalo litajumuisha Rais, Waziri Kiongozi, Mawaziri wengine pamoja na Wajumbe wengine isipokuwa tu jumla ya wajumbe wote kwa Baraza la Mapinduzi haitozidi ishirini kwa wakati mmoja.

(2) Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi watateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(3) Kazi za Baraza la Mapinduzi zitakuwa:-

(a) kumsaidia na kumshauri Rais katika mambo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

(b) kuamua na kutekeleza msimamo wa jumla na sera katika mambo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambayo hayako kwenye Muungano;

(c) kuratibu shughuli za Rais, Waziri Kiongozi na Wizara za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yao; na

(d) kutekeleza maamuru ya Chama kwa mujibu wa Katiba ya Chama pamoja na miongozo mengine ya Chama ambayo itatolewa mara kwa mara kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

(e) kuratibu, kuzungumza na kutekeleza maagizo ya Serikali ya Muungano kwa mambo ya Muungano yanayohusu Serikali ya Mapinduzi na ambayo yatatolewa mara kwa mara na Serikali ya Muungano au Chama.

(4) Baraza la Mapinduzi kwa pamoja litawajibika kwa Baraza la Wawakilishi pamoja na watu kwa ujumla kuhusiana na mambo yote yaliyotendwa na au kwa amri ya Rais au Waziri Kiongozi au Waziri mwengine katika utekelezaji wa shughuli zake za kikazi.

(5) Maelezo ya kijifungu (3) na (4) hayatatumika kuhusiana na:-

(a) kuteuliwa na kuachishwa kazi kwa Waziri Kiongozi, Mawaziri, Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi na Naibu Mawaziri chini ya kifungu 38,40,41 na 45 au kupewa dhamana kwa Waziri ye yote chini ya kifungu cha 42.

(b) kuvunjwa kwa Baraza la Wawakilishi au

(c) kuhusiana na mambo yaliyotajwa katika kifungu cha 57 (yanayohusiana na uwezo wa kutoa msamaha).

Ugawaji wa Wizara kwa Mawaziri.

42. (1) Majukumu kwa shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ikiwa ni pamoja na utawala wa Idara yo yote ya Serikali yanaweza kuwekwa kwa Waziri Kiongozi na Mawaziri wengine kama Rais atavyoidhinisha kwa maandishi.

(2) Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi ambao hawana Mawizara watakuwa Mawaziri wasio na Wizara maalum.

Mikutano ya Baraza.

43. (1) Rais akiwa ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ataongoza mikutano yote na ikiwa hayupo, Waziri Kiongozi atakuwa Mwenyekiti wa Muda.

(2) Iwapo Waziri Kiongozi naye hayupo Zanzibar basi mikutano itasimamiwa na mtu anayeshikilia madaraka ya Urais.

(3) Kiwango cha kufanyika mkutano wa Baraza la Mapinduzi itakuwa ni thuluthi mbili.

Viapo vya uaminifu.

44. Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi hataanza kufanya kazi zake, mpaka ale kiapo cha uaminifu na kiapo cha utekelezaji wa kazi zake kama vitavyowekwa na Baraza la Wawakilishi.

Naibu Mawaziri .

45. Rais anaweza kwa kushauriana na Waziri Kiongozi kuteua Naibu Mawaziri kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili kumsaidia Rais, Waziri Kiongozi na Mawaziri katika utekelezaji wa kazi zao.

Nafasi ya Waziri Memba wa Baraza la Mapinduzi kuwa wazi.

46. Nafasi ya Waziri, Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi na Naibu Waziri itakuwa wazi:-

(a) Endapo Rais atamwondosha kwenye madaraka hayo kwa hati yenye muhuri wa Serikali au

(b) iwapo mjumbe ameacha kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu nyengine zaidi ya kuvunjika kwa Baraza hilo; au

(c) endapo Rais atakubali ombi la kujiuzulu kwa mshika wadhifa huo; au

(d) mara kabla ya Rais kuanza kazi zake.

Katibu wa Baraza la Mapinduzi.

47. (1) Kutakuwa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi ataechaguliwa na Rais na ambaye ndiye atakayekuwa mdhamana wa ofisi ya Baraza hilo na mdhamana kwa mujibu wa maelekezo atakayopewa na Rais, wa kupanga shughuli za mikutano pamoja na kuweka kumbukumbu ya mikutano hiyo, na kupeleka maamuzi yanayohusika kwa watu au vyombo vinavyohusika, na atafanya kazi nyengine atakazopewa na Rais mara kwa mara.

(2) Katibu wa Baraza la Mapinduzi atakuwa ndiye Kiongozi wa Watumishi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Makatibu Wakuu.

48. (1) Pale Waziri Kiongozi au Waziri ye yote mwengine anapokuwa na dhamana ya Wizara yo yote ya Serikali, atakuwa ndiye msimamizi na dhamana Mkuu na bila ya kuathiri masharti yo yote ya usimamizi, Wizara ya Serikali itakuwa chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu ambaye ofisi yake itakuwa ni ya utumishi wa Serikali.

(2) Kutakuwa na Katibu Mkuu katika Afisi ya Rais na Katibu Mkuu katika Afisi ya Waziri Kiongozi.

(3) Makatibu Wakuu wote watateuliwa na Rais.

(4) Katibu wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu ye yote hatoanza kazi yake mpaka kwanza ale kiapo cha uaminifu na kiapo chengine cho chote cha utendaji wa kazi zake kama kitavyowekwa na Baraza la Wawakilishi.

## Sehemu ya nne
## Madaraka ya Serikali:

Madaraka ya Serikali ya Zanzibar.

49. Madaraka ya Serikali ya Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Rais, na kwa mujibu wa Katiba hii, anaweza kuyatekeleza yeye mwenyewe moja kwa moja au kuwapa viongozi walio chini yake kutekeleza madaraka hayo.

Ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika kifungu hiki hayazuii sheria kukabidhi madaraka ya kutekeleza kazi kwa chombo cho chote cha umma au kwa mtu mwengine ye yote ambaye si Rais wa Zanzibar.

Kutolazimika kwa Rais kufuata ushauri wa mtu.

50. Mbali na kuzingatia Siasa na maagizo ya Chama, Rais wa Zanzibar halazimiki kufuata ushauri atakaopewa na mtu ye yote katika utekelezaji wa shughuli zake, isipokuwa kama sheria inaagiza vinginevyo.

Uanzishwaji wa Afisi na wadhamini wa Afisi hizo.

51. Kwa mujibu wa Katiba hii na bila ya kuathiri masharti ya sura ya Nane au sheria nyengine yo yote iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi mamlaka:

(a) ya kuanzisha au kufuta ofisi katika Zanzibar, na

(b) ya kuteua Wakuu wa Ofisi hizo, na ya kupandisha cheo kwa muda wa utumishi, kufukuzwa na kushughulikia na hatua za kinidhamu kwa watu walioteuliwa kushika dhamana za ofisi hizo, yamo mikononi mwa Rais.

Muda wa kufanya kazi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

52. Isipokuwa kama imeelezwa vyenginevyo na Katiba hii au sheria yo yote nyengine kila mtu anaefanya kazi katika ofisi ya Serikali ya Zanzibar atashika dhamana hiyo hadi hapo Rais atakavyoamua vyenginevyo.

(2) Katika kifungu hiki "ofisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar maana yake ni ofisi ya Serikali", Kikosi Maalumu cha Kuzuwiya Magendo, Chuo cha Mafunzo au Jeshi la Kujenga Uchumi au shughuli nyengine yo yote ilioanzishwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mujibu wa Katiba hii na inajumuisha pia ofisi katika mashirika yote ya Serikali.

/26..

Mwanasheria Mkuu.

53.(1) Kutakuwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambae ofisi yake itakuwa ni ofisi ya utumishi ya Serikali na ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu hatafaa kuchaguliwa kuwa Mwanasheria Mkuu au kufanyakazi za Mwanasheria Mkuu mpaka awe na sifa za kumwezesha kuwa Mwanasheria katika Zanzibar na ambaye ana sifa hizo kwa muda usiopungua miaka saba.

Kazi za Mwanasheria Mkuu.

54.(1) Mwanasheria Mkuu ndiye atakayekuwa Mshauri Mkuu wa kisheria kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na atatekeleza shughuli nyengine zo zote za kisheria zitazopelekwa kwake au atakazoagizwa na Rais au kwa mujibu wa Katiba hii au sheria nyenginezo zo zote.

(2) Mwanasheria Mkuu atakuwa na uwezo wa kufanya haya yafuatayo ikiwa ataona ni muhimu kufanya:-

(a) kufungua na kushughulikia mashtaka yo yote ya jinai dhidi ya mtu ye yote mbele ya mahkama yo yote (isipokuwa ya kijeshi) kuhusiana na kosa lo lote ambalo mtu huyo anashtakiwa nalo.

(b) kuchukua na kuendeleza mashtaka yo yote ya jinai ambayo mwanzoni yalifunguliwa na mtu au chombo chengine; na

(c) kusimamisha mashtaka yo yote ya jinai ambayo yalianzishwa na mtu ye yote au chombo cho chote.

(3) Mwanasheria Mkuu anaweza kumtaka Kamishna wa Polisi kufanya uchunguzi juu ya jambo lo lote ambalo Mwanasheria Mkuu anaona kuwa linahusiana na kosa lo lote au linalodaiwa kuwa limetendewa au kosa linalotuhumiwa kuwa limetendeka, na Kamishna huyo atatimiza matakwa hayo na baadaye atariporti kwa Mwanasheria Mkuu kuhusu uchunguzi wake.

(4) Mamlaka ya utekelezaji wa kazi zake chini ya kijifungu (2)(a) na (3) yanaweza kutekelezwa na Mwanasheria Mkuu mwenyewe au na watu wengine walio chini yake kwa maagizo au amri maalum kutoka kwa Mwanasheria Mkuu.

(5) Mamlaka ya Mwanasheria Mkuu chini ya kifungu (b) na (c) ya kijifungu (2) yatakuwa mikononi mwake na hayataingiliwa na mtu ye yote au chombo cho chote.

Kwa kuzingatia kwamba pale ambapo mtu mwengine au chombo chengine kimefungua mashtaka ya jinai, basi hakuna cho chote katika kijifungu hiki kitakachozuia kufutwa kwa mashtaka hayo na mtu au chombi kilichoshtaki na kwa idhini ya mahkama.

(6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, rufaani yo yote kutokana na hukumu katika kesi ya jinai yo yote kwenye Mahkama yo yote au suala lo lote la kisheria lililowachwa kwa ajili ya mahtaka hayo kufikishwa kwenye mahkama nyengine, itahesabiwa kuwa ni sehemu ya mashtaka hayo.

Kwa kuzingatia kwamba yale mamlaka ya Mwanasheria Mkuu chini ya kijifungu (2) (c) hayatatekelezwa kuhusiana na rufaa yo yote ya mtu ambaye amehukumiwa katika kosa la jinai lo lote au kuhusiana na suala lo lote la kisheria lililowekwa makusudi kwa ajili ya mtu huyo.

(7) Katika kutumia uwezo wake chini ya kifungu hichi, Mwanasheria Mkuu atatilia maanani umuhimu wa Taifa kwa kutaka kuona haki inatekelezwa na nia yake ya kuzuia utumiaji mbaya wa vyombo vya kisheria.

Kiapo cha uaminifu

55. Mwanasheria Mkuu hatoanza kazi yake mpaka ale kiapo cha uaminifu na kiapo chengine cha utekelezaji wa kazi zake kama itakavyowekwa na Baraza la Wawakilishi.

Mshauri Maalum.

56. (1) Rais anaweza kumteua mtu yo yote kuwa ni Mshauri wake Maalum ili kumsaidia katika utendaji wa kazi zake.

(2) Uteuzi wo wote chini ya kifungu hiki utafanyika kama apendavyo Rais na hautaendelea tena iwapo mtu mwengine atashika madaraka ya Urais.

Uwezo wa kutoa msamaha.

57. Rais anaweza:-

(a) Kutoa msamaha bila ya masharti au kwa masharti kwa mtu ye yote aliyehukumiwa kwa kosa lo lote.

(b) kutoa uahirisho ama wa muda au wa moja kwa moja katika utekelezaji wa adhabu yo yote iliyotolewa na mahakama kwa mtu huyo kuhusiana na kosa alilotenda;

(c) kubadili adhabu aliyopewa mtu kutokana na kosa lo lote na kuifanya iwe ndogo zaidi;

(d) kusamehe kabisa au kwa kiasi fulani mtu ye yote aliyepewa adhabu kwa kosa lo lote au adhabu ya utaifishaji iliyotolewa na Serikali dhidi yake;

Kamati ya ushauri katika uwezo wa kutoa msamaha.

58. (1) Kutakuwa na Kamati ya ushauri kwa Rais katika uwezo wa kutoa msamaha ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwanasheria Mkuu akiwa ndiye Mwenyekiti;

(b) si chini ya wajumbe watatu na si zaidi ya wajumbe watano watakaoteuliwa na Rais, ambapo kati yao angalau mmoja atakuwa ni Waziri na angalau mmoja atakuwa ni mtu mwenye sifa za kuwa Daktari katika Zanzibar.

(2) Mjumbe wa Kamati aliyeteuliwa kwa mujibu wa kijifungu (1)(b) ataendelea na dhamana yake kwa kipindi kilichoainishwa kwenye amri iliyomteua.

Kwa kuzingatia kwamba kiti chake kitakuwa wazi:-

(i) ikiwa mtu huyo alipochaguliwa ni Waziri, pale atakapoachishwa uwaziri;

(ii) ikiwa Rais ataamuru hivyo kwa maandishi.

(3) Bila ya kutegemea kasoro katika jumla ya wanachama wote, Kamati hiyo inaweza kufanyakazi na shughuli zake hazitaathirika kwa kuwepo au kutokuwepo kwa mtu ye yote ambaye hawajibiki kuwepo au kushiriki katika Kamati hiyo.

(4) Kamati hiyo itapanga utaratibu wake wenyewe.

Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya.

59. (1) Kutakuwa na Mkuu wa Mkoa katika kila Mkoa wa Zanzibar ataeteuliwa na Rais kwa kushauriana na Rais wa Jamhuri ya Muungano.

(2) Kutakuwa na Mkuu wa Wilaya katika kila Wilaya ya Zanzibar ataeteuliwa na Rais.

(3) Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya aliyeteuliwa, kwa mpangilio chini ya kijifungu (1) na (2) cha kifungu hichi hatoanza kazi zake hadi kwanza ale kiapo cha uaminifu na kiapo cha utendaji wake wa kazi zake.

Kazi za Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya.

60. (1) Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya atakuwa ndiye mtendaji Mkuu; kwa kadiri itavyokuwa wa Mkoa ule au Wilaya ile.

(2) Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya anaweza, akipenda na bila kuathiri masharti yo yote katika Katiba hii au Sheria nyengine ye yote, kutoa madaraka yake kwa shughuli za zote za Serikali ya Mkoa huo au ya Wilaya hiyo, kwa kadiri itavyokuwa kwa mtu ye yote anaehisi anafaa, isipokuwa tu madaraka ya kuteua Kaimu Mkuu wa Mkoa au Wilaya yatakuwa mikononi mwa Rais.

SURA YA TANO
Baraza la Wawakilishi
Sehemu ya Kwanza
Muundo wa Baraza
la Wawakilishi

Baraza la Kutunga Sheria.

61. (1) Kutakuwa na Baraza la Kutunga Sheria litakalokuwa na sehemu mbili, Rais wa Zanzibar kwa upande mmoja na Baraza la Wawakilishi kwa upande wa pili.

(2) Iwapo, kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au masharti ya sheria nyengine, jambo lo lote linahitaji kuamuliwa au kutekelezwa na sehemu zote mbili za Baraza la Wawakilishi, basi jambo hilo halitakuwa na nguvu za kisheria mpaka liwe limeamuliwa au limetekelezwa na Baraza la Wawakilishi na vile vile na Rais.

Kuanzishwa kwa, na Muundo wa Baraza la Wawakilishi.

62. (1) Kutakuwa na Baraza la Wawakilishi ambalo, bila ya kuathiri masharti mengine yo yote yaliyomo katika Katiba hii litakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) wajumbe wa kuchaguliwa kutokana na kifungu cha 63 cha Katiba hii;

(b) Wajumbe wa kuteuliwa kutokana na kifungu cha 64 cha Katiba hii;

(c) Wajumbe waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi kutokana na kifungu cha 65 cha Katiba hii;

(d) wakuu wote wa Mikoa walioteuliwa katika Mikoa ya Zanzibar kwa mujibu wa kifungu cha 59 cha Katiba hii.

(2) Rais hatokuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Uchaguzi wa wajumbe wa kuchaguliwa.

63.(1) Zanzibar itagawanywa katika majimbo ya uchaguzi kutokana na kifungu cha 119 cha Katiba na kila jimbo moja la uchaguzi litachagua mtu mmoja kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa njia ambayo itaelezwa na Katibu au chini ya sheria nyingine yo yote.

(2) Kila mtu ambaye amejiandikisha katika jimbo la uchaguzi kama ni mpiga kura wa kumchagua mjumbe, isipokuwa awe amewekwa kizuizini kwa njia ya halali au hafai kutokana na sheria kupiga kura katika uchaguzi huo kwa njia ambayo amekutikana na kosa lenye kuhusiana na uchaguzi au kwa njia ambayo imeripotiwa kuwa amepatikana na kosa hilo katika mahkama au kujaribu kubatilisha uchaguzi, atastahiki kupiga kura katika jimbo la uchaguzi hilo kwa mujibu wa sheria iliyowekwa.

(3) Uandikishaji wa kupiga kura wa wajumbe wa kuchaguliwa na uendeshaji wa uchaguzi huo utaongozwa na kusimamiwa na Tume ya Uchaguzi.

Wajumbe wa kuteuliwa.

64. Kutakuwa na wajumbe kumi wa kuteuliwa wa Baraza la Wawakilishi ambao watateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu ambao akiteuliwa atafaa kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Wajumbe wa kuchaguliwa na Baraza la Wawakilishi

65. Kutakuwa na wajumbe watano wanawake wa Baraza la Wawakilishi ambao ni Wa-Zanzibari watakochaguliwa na Baraza la Wawakilishi kupitia Jumuia ya Wanawake Tanzania kutoka Zanzibar.

Sifa za kuchaguliwa.

66. Mtu atafaa kuchaguliwa kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwa, na hatofaa kuchaguliwa mpaka, siku ya kuchaguliwa kwake katika uchaguzi:-

(a) awe ni Mzanzibar aliyetimia umri wa miaka ishirini na moja.

(b) awe amejiandikisha au ana sifa za kujiandikisha katika jimbo la uchaguzi kama mpiga kura katika uchaguzi wa Baraza la Wawakilishi.

(c) awe anaweza kusoma na isipokuwa awe hana uwezo wa kuona au ana magonjwa mengine ya kiwiliwili, anasema lugha ya Kiswahili;

(d) awe ni mwanachama wa Chama mwenye kutimiza masharti ya uwanachama kama yalivyoelezwa katika Katiba ya Chama;

(e) awe ni mtu ambaye hakuzuiliwa kugombea uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki au kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ama Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Kutofaa kuchaguliwa. 67. (1) Hakuna mtu atakaechaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(a) ikiwa mtu huyo ana uraia wa nchi nyingine yo yote;

(b) ikiwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi au Bunge la Jamhuri ya Muungano imethibitishwa rasmi kwamba mtu huyo ana ugonjwa wa akili;

(c) ikiwa:-

(i) mtu huyo amehukumiwa na Mahkama yo yote Zanzibar au katika Jamhuri ya Muungano na kupewa adhabu ya kifo au kufungwa Chuo cha Mafunzo au Gerezani, kwa muda wa miezi sita; au

(ii) mtu huyo amewekwa kizuizini kwa mujibu wa Sheria ya Kuwekwa kizuizini ya Jamhuri ya Muungano au Sheria ya Zanzibar na amekaa kizuizini kwa mujibu wa amri hiyo kwa muda unaozidi miezi sita; au

(iii) mtu huyo amesafirishwa kwa lazima kisheria kwa mujibu wa amri iliyotolewa kwa mujibu wa masharti ya sheria ya Usafirishaji wa lazima na iwapo amekaa huko alikopelekwa kwa muda unaozidi miezi sita na mpaka wakati huo amri hiyo bado haijabatilishwa;

(d) ikiwa mtu huyo ana masilahi yo yote katika mkataba wa Serikali wa aina yo yote iliyowekwa miiko maalum kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi na iwapo amekiuka miiko hiyo;

(e) ikiwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi mtu huyu amezuiliwa kuwa mjumbe katika Baraza la Wawakilishi kwa sababu kwamba ameshika madaraka katika utumishi, wa Serikali ya Zanzibar na sheria hiyo imetamka wazi kuwa ni mwiko kwa mtu huyo kuwa mjumbe katika Baraza la Wawakilishi;

(f) ikiwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi inayoshughulikia makosa yanayohusika na uwakilishi wa aina yo yote mtu huyo amezuiliwa kuwa mwakilishi;

(g) ikiwa mtu huyo, au kadri itakavyokuwa, mke wake au mume wake ana hisa au masilahi mengineyo yoyote ya aina hiyo katika kampuni yo yote;

(h) ikiwa mtu huyo, au kadri itakavyokuwa, mke wake au mume wake, ni Mkurugenzi katika Kampuni yoyote ya kibepari au ya kikabaila;

(i) ikiwa mtu huyo, au kadri itavyokuwa, mke wake au mume wake, ana nyumba ya kupangisha;

(j) ikiwa mtu huyo, au kadri itavyokua mke wake au mume wake, hupata riziki yake kwa kuajiri watu wengine kama itakavyofafanuliwa na sheria itayotungwa na Baraza la Wawakilishi;

/34..

Isipokuwa kwamba mtu huyo hatahesabiwa kuwa amepoteza sifa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwa mtu huyo anamwajiri mtu mwingine kwa ajili ya kufanyakazi za msimu na huyo mtu alieajiriwa hulipwa kwa kutwa kwa kufuata muda aliofanya kazi au kazi maalum aliyofanya.

(2) Mtu hawezi kugombea kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwa wakati huo yeye ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

(3) Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti yatakayomzuia mtu kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi muda wo wote utakaotajwa na Baraza la Wawakilishi (ili mradi muda huo usizidi miaka mitano) ikiwa mtu huyo atapatikana na hatia mbele ya mahkama kwa ajili ya aina yo yote ya makosa yatakayotajwa katika sheria hiyo yanayohusika na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(4) Kwa madhumuni ya kutoa fursa ya kukata rufaa kwa mujibu wa sheria kwa mtu ye yote aliyethibitishwa na kupewa adhabu ya kifo au ya kufungwa Chuo cha Mafunzo au Gerezani aliepatikana na hatia ya kosa lolote lililotajwa katika sheria kwa mujibu wa kifungu (3) cha kifungu hiki, Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga kwa ajili ya kuweka masharti yatakayoeleza kwamba hiyo hukumu inayopingwa na mtu huyo haitakuwa na nguvu kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya kijifungu (1) au ya (3) ya kifungu hiki mpaka upite kwanza muda utakaotajwa katika sheria hiyo.

(5) Kanuni zifuatazo zitatumika kwa ajili ya ufafanuzi wa aya ya (c) ya kijifungu (1) ya kifungu hiki, yaani:-

(a) Ikiwa mtu amepata adhabu mbili au zaidi za kufungwa muda wa mfululizo, basi adhabu hizo zitahisabiwa kuwa ni adhabu mbali mbali iwapo muda uliotajwa katika moja ya adhabu hizo hauzidi miezi sita, lakini iwapo muda uliotajwa katika adhabu yoyote kati ya adhabu hizo unazidi miezi sita basi adhabu hizo zote zitahesabiwa kama ni adhabu moja;

(b) ikiwa mtu amepewa adhabu ya kufungwa Chuo cha Mafunzo au Gerezani akifahamika kuwa adhabu hiyo ya kufungwa imetolewa badala ya adhabu ya kutozwa faini au imetolewa kwa sababu mtu huyo ameshindwa kulipa faini aliyoamrishwa kulipa, basi muda wa kifungo cha namna hiyo hautahesabiwa.

(6) Katika aya ya (d) ya kijifungu (1) ya kifungu hiki mkataba wa Serikali maana yake ni mapatano yoyote ya mkataba ambayo mmoja wapo wa walioshiriki ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au idara yoyote ya Serikali au mtumishi yoyote wa Serikali aliyeshiriki kwa niaba ya Serikali.

(7) Kwa ajili ya ufafanuzi wa aya ya (g) ya kifungu (1) ya kifungu hiki "hisa" ifahamike kwa maana ya kawaida ya neno hilo na vile vile ni pamoja na hati ya dhamana au ya aina ya stakabadhi ya fedha iliyowekwa akiba au iliyokopeshwa, na pia faida au mali nyingine yoyote.

(8) Kanuni zifuatazo zitatumika kwa ajili ya ufafanuzi wa aya ya (g) ama aya ya (i) ya kijifungu (1) ya kifungu hiki yaani:-

(a) mtu hatahesabiwa kuwa ana hisa katika Kampuni au kuwa ana nyumba ya kupangisha au kuwa ana maslahi mengineyo yoyote katika kampuni yoyote au nyumba yoyote ikiwa mali au maslahi aliyonayo amepata kutokana na mali waliyoshikia wadhamini kwa niaba yake au amepata kwa mujibu wa masharti ya wakfu na ikiwa:-

(i) yeye mwenyewe hakuwa miongoni mwa wale watu waliofanya mipango ya kukabidhi mali kwa wadhamini wala mipango ya kuweka wakfu; na

(ii) iwapo mali au maslahi aliyonayo amepata baada ya siku ya kwanza tangu kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi lakini kabla ya mtu huyo au kadri itakavyokuwa mke wake au mume wake, kushika madaraka yake kama Mjumbe Mwakilishi, basi mtu huyo awasilishe kwenye Tume ya Uchaguzi ya Tanzania Visiwani tamko rasmi katika fomu maalumu itakayotumiwa kwa ajili hiyo kwamba ataondokana na mali hiyo au maslahi hayo kabla ya kumalizika miezi mitatu tangu siku ambayo mtu huyo, au kadiri itakavyokuwa mke wake au mume wake, atakavyoshika madaraka yake kama Mjumbe Mwakilishi.

(9) Kanuni zifuatazo zitatumika kwa ajili ya ufafanuzi wa aya ya (j) ya kijifungu (1) yaani:-

(i) malipo yanayotolewa kwa mtu kama ujira wake kwa ajili ya kazi anazotekeleza kama Mjumbe Mwakilishi, lakini siyo pamoja na posho yoyote anayolipwa kama Mjumbe Mwakilishi;

(ii) mapato yanayotokana na shughuli zake kama mkulima au kama mfanyakazi;

(iii) ujira anaolipwa mtu kwa mujibu wa mapatano ya mkataba wa kazi;

(iv) mali anayopata mtu kutoka kwa wadhamini wanaoshikilia mali kwa niaba yake kwa mujibu wa dhamana au wakfu;

(b) ikiwa mtu anapokea mishahara miwili au zaidi, basi atahesabiwa kuwa anapokea mshahara mmoja tu iwapo jumla ya fedha yote anayopokea haizidi kiwango cha mshahara anaolipwa Mjumbe Mwakilishi;

(c) Mtu ye yote anayepokea mshahara hatapoteza sifa za kugombea kuwa Mjumbe Mwakilishi kwa sababu tu kwamba akichaguliwa ataendelea kupokea mshahara wake na vile vile atakuwa na haki ya kulipwa mshahara kama Mjumbe Mwakilishi, lakini mtu huyo atalazimika, kabla ya kushika madaraka yake kama Mjumbe Mwakilishi, kuwasilisha kwa Spika, tamko rasmi katika fomu maalum atakayotumiwa kwa ajili hiyo kwa mujibu wa sheria hii kwamba:-

(i) ataacha kupokea mmoja wapo wa mishahara hiyo miwili; au

(ii) atapokea sehemu tu ya mshahara anaostahili kulipwa kama Mjumbe Mwakilishi ili kwamba sehemu hiyo ikichanganywa na ule mshahara wake mwingine jumla ya fedha yote haitazidi kiwango cha mshahara anaolipwa Mjumbe Mwakilishi; na

(10) Kwa ajili ya ufafanuzi wa maelezo kuhusu sifa za uchaguzi yaliyomo katika vifungu vifuatavyo, kila itakapotajwa chini ya Katiba hii kwamba utekelezaji wa jambo lo lote unahitaji mtu mwenye sifa za uongozi au mtu ambaye hakupoteza sifa za uongozi, basi ila iwapo maelezo yanahitajia vinginevyo, ifahamike kuwa sifa zinazohusika ni zile zinazomwezesha mtu kuchaguliwa kuwa Mjumbe Mwakilishi au Baraza la Mapinduzi kama viongozi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama ilivyoelezwa katika vifungu mbali mbali vya Katiba hii miongoni mwao ikiwa:-

(a) Ni mwiko kwa kiongozi kutumia madaraka aliyopewa kwa ajili ya manufaa yake binafsi, au kwa upendeleo, au kwa namna yo yote ambayo ni kinyume na lengo lililokusudiwa madaraka hayo;

(b) ni mwiko kwa kiongozi kupokea kipato cha kificho, au rushwa au kushiriki katika mambo yo yote ya magendo; na

(c) kiongozi aliyeachishwa uongozi hatakuwa na haki ya kuomba tena nafasi ya uongozi mpaka ipite miaka mitano tangu alipoachishwa hivyo.

Iapo cha jumbe wakilishi.

68. Kila Mjumbe Mwakilishi atatakiwa kuapishwa, katika Baraza la Wawakilishi, kiapo cha uaminifu kama kitavyowekwa na Baraza la Wawakilishi; lakini Mjumbe Mwakilishi anaweza kushiriki katika uchaguzi wa Spika, hata kabla hajaapishwa.

amko rasmi la Wajumbe wakilishi husu masharti ya ongozi.

69. (1) Kila Mjumbe Mwakilishi atatakiwa kabla ya kumalizika siku kumi na tano tangu ashike madaraka katika Baraza la Wawakilishi kama Mjumbe Mwakilishi, kuwasilisha kwa Spika nakala mbili za tamko rasmi kwamba yeye hajapoteza sifa za kuendelea kuwa Mjumbe Mwakilishi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa chini ya Katiba hii kama sifa za kuwa Mjumbe Mwakilishi.

(2) Tamko rasmi linalotakiwa kuwasilishwa kwa Spika kwa mujibu wa masharti ya ibara hii litatolewa kwa kutumia fomu maalumu kwa itakayowekwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(3) Spika, atawasilishwa kwa Mwenyekiti wa Tume ya Tabia ya Viongozi nakla moja ya kila tamko rasmi lililowasilishwa kwake kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki.

jumbe wa araza la wakilishi toa taarifa a mali.

70. (1) Kila Mjumbe Mwakilishi anayehusika na masharti ya kifungu hiki atatakiwa kuwasilisha kwa Spika, wa Baraza la Wawakilishi nakala mbili za taarifa rasmi ya maelezo ya mali yake na kadri itakavyokuwa, mali ya mke wake au mume wake. Taarifa hiyo itatolewa kwa kutumia fomu maalum itakayotumika maalumu kwa kazi hiyo kwa mujibu wa Katiba hii.

(2) Spika, atawasilisha kwa Mwenyekiti wa Tume ya Tabia ya Viongozi nakala moja ya kila taarifa rasmi iliyowasilishwa kwake kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki.

(3) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti kwa makusudi ya kuhifadhi kama siri kila taarifa ya mali iliyowasilishwa na Mjumbe Mwakilishi kwa mujibu wa masharti ya kifungu na masharti hayo yaweza kueleza mambo yafuatayo:-

(a) kwamba taarifa ya mali yaweza kutolewa tu ikiwa inahitajiwa kama ushahidi mbele ya Mahkama Kuu wakati inaposikiliza shauri lililofunguliwa katika Mahkama Kuu kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii kuhusu masharti ambayo Mahkama Kuu ina mamlaka kusikiliza juu ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi;

(b) Kwamba kabla taarifa ya mali haijatolewa kama ushahidi mbele ya Mahakama Kuu, watu pekee wanaoweza kuona taarifa hiyo au kujua yaliyomo katika taarifa hiyo ni Rais wa Zanzibar, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na Wakuu wengine walioruhusiwa kwa mujibu wa sheria hiyo;

(c) mambo mengine yo yote ambayo yatahakikisha kwamba watu wasioruhusiwa au wasiohusika hawapati nafasi ya kuona taarifa ya mali kujua yaliyomo katika taarifa ya mali.

Muda wa wajumbe Wawakilishi kushika madaraka yao.

71. (1) Mjumbe Mwakilishi ataacha kuwa Mjumbe Mwakilishi na ataacha kiti chake katika Baraza la Wawakilishi litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo:-

(a) ikiwa litatokea jambo lo lote ambalo, kama asingekuwa Mjumbe Mwakilishi lingemfanya mtu huyo asiwe na sifa za kuwa Mjumbe Mwakilishi au apoteze sifa za uongozi.

Isipokuwa kwamba iwapo Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au kadiri itakavyokuwa, mke au mume wake amepata mali au maslahi mengineyo yo yote yaliyotokana na haki ya kumiliki nyumba na ikiwa mali au maslahi hayo amepata kwa njia ya urithi, au kwa mujibu wa sheria, basi Mjumbe Mwakilishi huyo hataacha kiti chake katika Baraza la Wawakilishi kwa sababu ya masharti yaliyowekwa chini ya Katiba hii kama Mjumbe Mwakilishi huyo, au kadri itakavyokuwa mke wake au mume wake atachukua hatua hizi kuonekana na mali au maslahi hayo kabla ya kumalizika miezi mitatu tangu mali hiyo au maslahi yaliyopatikana.

(b) ikiwa Mjumbe Mwakilishi huyo atachaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar;

(c) kwa Mjumbe Mwakilishi asiye Mkuu wa Mkoa, ikiwa atakosa kuhudhuria vikao vya Mikutano ya Baraza la Wawakilishi vitatu mfululizo bila ya ruhusa ya Spika;

(d) iwapo Mjumbe Mwakilishi au kadri itakavyokuwa, mke au mume wake, ametoa tamko rasmi kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii kuhusu sifa za kuwa Mjumbe Mwakilishi katika Baraza la Wawakilishi, basi ikiwa Mjumbe Mwakilishi huyo au kadri itakavyokuwa mke wake au mume wake, atashindwa kutimiza yaliyomo katika tamko hilo;

(e) kwa Mjumbe Mwakilishi ambaye anatakiwa kutoa tamko rasmi kuhusu masharti ya uongozi kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, ikiwa litatokea lo lote kati ya mambo yafuatayo:

(i) ikiwa atashindwa kutoa hilo tamko rasmi kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii katika muda uliowekwa mahsusi kwa ajili hiyo; au

(ii) ikiwa atapatikana na hatia kwa kosa la kutoa habari za uwongo kwa kiapo kinyume na Sheria ya Kanuni za Jinai, kuhusu hilo tamko rasmi;

(f) kwa Mjumbe Mwakilishi ambaye anatakiwa kutoa taarifa rasmi ya mali kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, ikiwa atashindwa kutoa hilo tamko rasmi katika muda uliowekwa mahususi kwa ajili hiyo kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi lakini iwapo Mjumbe Mwakilishi hataacha kuwa Mjumbe Mwakilishi kwa mujibu wa jambo lo lote kati ya mambo hayo yaliyotajwa na kama hatajiuzulu au kufariki mapema zaidi basi Mjumbe Mwakilishi ataendelea kushika madaraka yake kama Mjumbe Mwakilishi mpaka Baraza la Wawakilishi litakapovunjwa.

(g) baada ya Baraza la Wawakilishi kuvunjwa;

(h) iwapo Mahkama Kuu au Mahkama ya Rufaani itaamuru Mjumbe apoteze kiti chake kwa mujibu wa kifungu 72 cha Katiba hii;

(i) ikiwa Mjumbe, kwa maandishi yake na ayatume kwa Spika atajiuzulu kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(2) Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka masharti yatakayomwezesha Mjumbe Mwakilishi kukata rufaa, kwa mujibu wa sheria kupinga hukumu ya kuthibitishwa kwake kuwa ni mtu mwenye ugonjwa wa akili au kupinga adhabu ya kifo au ya kufungwa Chuo cha Mafunzo au Gerezani au kupinga kupatikana kwake na hatia kwa kosa la aina iliyotajwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 67 cha Katiba hii au kosa la kutoa habari za uwongo kwa kiapo kinyume na Sheria ya Kanuni za jinai, kuhusu tamko rasmi

lilitolewa kwa mujibu wa masharti ya aya (f) ya kijifungu (1) ya kifungu hiki, na sheria hiyo inaweza kueleza kwamba hiyo hukumu inayopingwa na huyo Mjumbe Mwakilishi haitatiliwa nguvu kisheria mpaka umalizike kwanza muda utakaotajwa katika sheria hiyo.

Uamuzi wa suala kama mtu ni Mjumbe Mwakilishi ama sio.

72. (1) Mahkama Kuu ya Zanzibar ndiyo pekee yenye mamlaka ya kusikiliza shauri na kuamua suala kuhusu mambo yafuatayo:-

(a) kama uteuzi wa mtu ye yote kuwa Mjumbe Mwakilishi ulikuwa halali au sivyo; au

(b) kama Mjumbe Mwakilishi amekoma kuwa Mjumbe Mwakilishi na kiti chake katika Baraza la Wawakilishi kiwazi au hapana;

(2) Katika kusikiliza suala lo lote chini ya kifungu hiki Mahkama Kuu itakamilika pale tu itapokuwa na Majaji wasiopungua watatu.

Isipokuwa kwamba iwapo Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano imemtangaza Mjumbe Mwakilishi ye yote kwamba amechaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano au Tume ya Uchaguzi ya Tanzania Visiwani imemtangaza Mjumbe Mwakilishi yeyote kuwa amechaguliwa kuwa Rais basi Mahkama Kuu haitachunguza zaidi suala lo lote linalohusu kiti cha Mjumbe Mwakilishi huyo kuwa wazi.

(3) Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusu mambo yafuatayo:-

(a) watu wanaoweza kufungua shauri katika Mahkama Kuu kwa ajili ya kupata uamuzi juu ya suala lo lote kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki;

(b) sababu na nyakati za kufungua shauri au namna hiyo, utaratibu wa kufungua shauri na masharti yanayotakiwa yatimizwe kwa kila shauri kama hilo; na

(c) kutaja makala ya Mahkama Kuu juu ya shauri la namna hiyo, na kueleza utaratibu wa kusikiliza shauri lenyewe.

Spika.

73. (1) Kutakuwa na Spika wa Baraza la Wawakilishi ambaye atachaguliwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka miongoni mwa watu ambao ni wajumbe wa Baraza la Wawakilishi au wenye sifa za kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(2) Memba wa Baraza la Mapinduzi, Waziri Kiongozi, Waziri, Naibu Waziri, Mkuu wa Mkoa au mtu mwenye madaraka ya aina nyingine yo yote yatayotajwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi kwa madhumuni ya kifungu hiki, hataweza kuchaguliwa kuwa Spika.

(3) Mtu ambaye atakuwa ameshika madaraka ya Spika kwa mujibu wa kijifungu (1) ya kifungu hiki atatakiwa kuwasilisha kwa Rais nakala mbili za tamko rasmi kwamba hajapoteza sifa zinazotakiwa kuwa Mjumbe Mwakilishi kabla ya siku kumi na nane kumalizika tangu kuchaguliwa kwake. Tamko hilo litatolewa kwa kutumia fomu maalum itakayowekwa kwa mujibu wa Katiba hii.

(4) Rais atawasilisha kwa Mwenyekiti wa Tume ya Tabia ya Viongozi nakala moja ya kila tamko rasmi lililowasilishwa kwake kwa mujibu wa masharti ya kijifungu (3) ya kifungu hiki.

(5) Spika atatakiwa kuwasilisha kwa Rais nakala mbili za taarifa rasmi ya maelezo ya mali ya huyo Spika na kadri itakavyokuwa, mali ya mke wake au mume wake.

Spika atatoa taarifa hiyo kwa kutumia fomu maalum iliyowekwa kwa ajili hiyo kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi na atatoa taarifa ya namna hiyo kwa mara kadri itakavyoagiza sheria hiyo.

(6) Spika ataacha kuwa Spika na ataacha kiti cha Spika litakapotokea lo lote kati ya mambo yafuatayo:-

(a) iwapo mtu huyo alichaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi basi ikiwa ataacha kuwa Mjumbe Mwakilishi kwa sababu yo yote ambayo haihusiki na kuvunjwa kwa Baraza la Wawakilishi; au

(b) ikiwa kutatokea jambo lo lote ambalo, kama asingekuwa Spika lingemfanya mtu huyo asiwe na sifa za kuwa Mjumbe Mwakilishi au apoteze sifa za uchaguzi wa Spika; au

(c) ikiwa mtu huyo ataondolewa kwenye madaraka ya Spika kwa azimio la Baraza la Wawakilishi lililoungwa mkono na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote; au

(d) ikiwa mtu huyo atashindwa kuwasilisha kwa Rais taarifa rasmi kwa mujibu wa masharti ya kijifungu (5) cha kifungu hichi; au

(e) ikiwa mtu huyo atapatikana na hatia kwa kosa la kutoa habari za uwongo, kwa kiapo, kinyume cha sheria ya Kanuni za Jinai, kuhusu tamko rasmi lo lote lililotolewa kwa mujibu wa masharti ya kijifungu (3) cha kifungu hiki.

(f) ikiwa mtu huyo atashindwa kuwasilisha kwa Rais tamko la mali kwa mujibu wa masharti ya kijifungu(3) ya kifungu hiki kabla ya kumalizika muda uliowekwa kwa ajili hiyo kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(7) Hakuna shughuli itakayotekelezwa katika Baraza la Wawakilishi (isipokuwa uchaguzi wa Spika) wakati wo wote ambao kiti cha Spika kitakuwa wazi, lakini kijifungu hiki, hakitozuwia Kamati za Baraza la Wawakilishi kufanya shughuli zao.

(8) Mtu ye yote ambaye si Mjumbe Mwakilishi, atakayechaguliwa kuwa Spika, atatakiwa, kabla ya kuanza kutekeleza madaraka yake, kuapishwa katika Baraza la Wawakilishi kiapo cha uaminifu.

ibu
pika.

74. (1) Kutakuwa na Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi ambaye atachaguliwa na Baraza la Wawakilishi kutokana na kanuni za Baraza ambaye atakuwa ni Mjumbe Mwakilishi ambaye hatokuwa Waziri Kiongozi, Waziri, Naibu Waziri, Mkuu wa Mkoa au Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi.

(2) Baraza la Wawakilishi litamchagua Naibu Spika:-

(a) chini ya masharti ya kifungu cha 73(7) katika mkutano wake wa mwanzo baada ya kuvunjwa Baraza; na

(b) litakapokutana Baraza kwa mara ya mwanzo wakati kiti cha Naibu Spika kiwazi kwa njia ambayo sio sababu ya kuvunjwa kwa Baraza, au kwa haraka iwezekanavyo;

(3) Kiti cha Naibu Spika kitakuwa wazi:-

(a) ikiwa Baraza la Wawakilishi ni mara yake ya mwanzo kukutana toka kuvunjwa kwa Baraza lilopita;

(b) ikiwa amechaguliwa kuwa Rais au Waziri Kiongozi, au Waziri, Naibu Waziri au Mkuu wa Mkoa au Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi.

/46..

(c) ikiwa amesita kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa njia ambayo sio kwa kuvunjwa Baraza; au

(d) ikiwa Baraza la Wawakilishi limeamua kwa uamuzi wa kura zisizopungua thuluthi mbili za wajumbe wote kuwa Naibu Spika huyo aondolewe katika kiti hicho.

Taratibu za uchaguzi wa Spika na Naibu Spika.

75. Katika Uchaguzi wo wote wa Spika au Naibu Spika kura za Wajumbe wa Baraza zitakuwa za siri.

Katibu wa Baraza la Wawakilishi.

76. (1) Kutakuwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi atakayeteuliwa na Rais wa Zanzibar.

(2) Afisi ya Katibu wa Baraza la Wawakilishi na afisi za wafanyakazi wake zitakuwa ni Afisi katika huduma ya Serikali.

(3) Katibu wa Baraza la Wawakilishi hatoanza kazi yake ila kwanza ale kiapo cha uaminifu na kiapo chengine cho chote kitachowekwa na sheria.

Sekretariet ya Baraza Wawakilishi

77. (1) Kutakuwa na Sekreteriet ya Baraza la Wawakilishi itayokuwa na nafasi za madaraka katika utumishi wa Serikali kwa idadi atakayoagiza Rais.

(2) Sekreteriet hiyo itakuwa na watumishi ambao idadi yao ngazi zao za utumishi zitaamuliwa na Tume ya uajiri Serikalini kwa kushauriana na Spika wa Baraza.

(3) Sekreteriet ya Baraza, chini ya uongozi wa Katibu wa Baraza itatekeleza kazi na shughuli zote zilizowekwa au zitazowekwa na sheria kwa ajili ya kuhakikisha utekelezaji bora wa shughuli za Baraza.

## Sehemu ya Pili

## Sheria na Taratibu Katika Baraza la Wawakilishi

Nguvu za kutunga Sheria.

78. (1) Nguvu za kutunga sheria kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muungano katika Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Baraza la Kutunga Sheria.

(2) Bila ya kuathiri masharti mengine ya Katiba hii, nguvu za Kutunga Sheria katika Baraza la Wawakilishi itakuwa kwa kupitishwa Miswada katika Baraza la Wawakilishi.

(3) Wakati Muswada umepitishwa na Baraza la Wawakilishi utapelekwa kwa Rais kwa kupata kibali chake.

(4) Iwapo Muswada ambao umepitishwa na Baraza la Wawakilishi umepelekwa kwa Rais wa Zanzibar na kupata kibali hicho, utakuwa sheria na hivyo utachapishwa katika Gazeti Rasmi.

(5) Baraza la Wawakilishi linaweza kuahirisha kuanza kutumika kwa sheria iliyotungwa, na bila kuathiri masharti ya kifungu cha 13 cha Katiba hii linaweza kufanya sheria kuanzia siku za nyuma.

(6) Sheria inayotungwa na Baraza la Wawakilishi itajulikana kuwa ni "Sheria ya Baraza la Wawakilishi" na jina la utunzi litakuwa "Imetungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar".

Taratibu za kutunga Sheria.

79. (1) Baada ya Muswada kuwasilishwa kwa Rais kwa ajili ya kupata kibali chake, Rais anaweza ama kukubali au kukataa kuukubali, na iwapo, atakataa kuukubali Muswada, basi ataurudisha kwenye Baraza la Wawakilishi pamoja na maelezo ya sababu zake za kukataa kuukubali Muswada huo.

/48..

(2) Baada ya Muswada kurudishwa kwenye Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Masharti ya kifungu hiki, hauwezi kupelekwa tena kwa Rais kwa ajili ya kupata kibali chake kabla ya kumaliza muda wa miezi sita tangu uliporudishwa, isipokuwa kama katika hatua yake ya mwisho kwenye Baraza la Wawakilishi kabla haujapelekwa tena kwa Rais Muswada huo umeungwa mkono na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote.

(3) Iwapo Muswada umerudishwa kwenye Baraza la Wawakilishi na Rais, halafu ukaungwa mkono kwenye Baraza la Wawakilishi na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote kama ilivyoelezwa katika kijifungu cha (2) na kupelekwa kwa Rais kwa ajili ya kupata kibali chake kwa mara ya pili kabla haujamalizika muda wa miezi sita tangu uliporudishwa, basi Rais atatakiwa kuukubali Muswada huo kabla ya kumalizika muda wa siku ishirini na moja tangu Muswada huo ulipowasilishwa kwake la sivyo basi itabidi alivunje Baraza la Wawakilishi.

(4) Masharti yaliyomo katika kijifungu hiki au katika kifungu cha 78(1) cha Katiba hii hayatalizuia Baraza la Wawakilishi kutunga sheria ya kuweka masharti ambayo yanaweza kukabidhi kwa mtu ye yote au kwa Idara yo yote ya Serikali madaraka ya kuweka kanuni zenye nguvu za kisheria au kuzipa nguvu za kisheria kanuni zo zote zilizowekwa na mtu ye yote au idara yo yote ya Serikali.

Kubadilisha Katiba.

80. (1) Kwa masharti ya kifungu hiki Baraza la Wawakilishi linaweza kubadilisha kifungu cho chote katika Katiba hii.

/49..

(2) Muswada wa Baraza la Wawakilishi wa kubadilisha Katiba hii hautopitishwa na Baraza isipokuwa uwe umeungwa mkono kwa mara ya kwanza na mara ya pili katika kusomwa kwa kura si chini ya theluthi mbili ya kura zote za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(3) Katika kifungu hiki:-

(a) marejeo katika Katiba hii ni marejeo katika Katiba kama itakavyorekebishwa mara kwa mara; na

(b) marejeo ya kubadilisha Katiba hii ni marejeo ya kufanya marekebisho, masahihisho au kutunga ikiwa na mabadiliko au kutokuwa na mabadiliko au masahihisho katika kifungu cho chote cha Katiba hii, kusimamisha au kufuata kifungu hicho na utungaji wa kifungu tofauti katika mahala pa kifungu cha zamani.

Uongozi wa Kikao wa Baraza la Wawakilishi.

81. Kila kikao cha Baraza la Wawakilishi kitaongozwa na:-

(a) Spika; au
(b) ikiwa hayupo Naibu Spika; au
(c) ikiwa Spika hayupo na Naibu Spika hayupo Mjumbe mwingine wa Baraza la Wawakilishi (asiyekuwa Waziri Kiongozi, Waziri, Naibu Waziri, Mjumbe wa Baraza la **Mapinduzi** au Mkuu wa Mkoa) **kama** Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watakao mchagua kwa ajili hiyo.

Viti vilivyo wazi katika Baraza la Wawakilishi na utaratibu wa kuendesha shughuli za Baraza.

82. (1) Baraza la Wawakilishi linaweza kuendesha shughuli bila kujali kuweko kwa kiti wazi kuhusu Mjumbe kuhusiana na kiti ambacho hakikujazwa wakati Baraza ndio kwanza liitishwe au kuundwa kwa mara ya kwanza na shughuli hizo zitaendelea bila ya kujali kuweko kwa mtu asiyehusika kuwepo au kupiga kura katika Baraza au kuwepo katika shughuli zinazoendelea.

(2) Bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika kifungu cha 80 cha Katiba hii idadi ya wajumbe kufanya mkutano itakuwa nusu ya Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi.

igaji ra tika raza la wakilishi.

83. (1) Isipokuwa imeelezwa vingine katika Katiba hii suala lo lote au uamuzi katika Baraza la Wawakilishi utaamuliwa kutokana na idadi kubwa ya Wajumbe walichudhuria kwenye kikao na kupiga kura.

(2) Jambo lo lote litakalopelekwa kwa uamuzi katika Baraza la Wawakilishi mtu atakayekuwa anaongoza kikao cha Baraza la Wawakilishi:-

(a) ikiwa ni Spika, atakuwa na kura ya uamuzi na siyo kura ya asili;

(b) ikiwa siye Spika, atakuwa na kura ya uamuzi pamoja na kura ya asili;

(3) Kanuni za Baraza la Wawakilishi zinaweza kuweka vifungu ambavyo Mjumbe ambaye anapiga kura na huku akiwa na hisa fulani ya jambo linalopigiwa kura asiwe na kura.

dareka a Rais tika raza la wakilishi.

84. Rais atahusika katika mamlaka ya shughuli zake kama Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhutubia Baraza la Wawakilishi wakati atakaoona unafaa kufanya hivyo.

mati za raza la wakilishi.

85. (1) Kutakuwa na Kamati za Kudumu katika Baraza la Wawakilishi zifuatazo:-

(a) Kamati ya Uongozi

(b) **Kamati** ya Fedha na Uchumi

(c) Kamati za Mambo ya Siasa

(d) Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali

(e) Kamati ya Mambo ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii,

(f) Kamati ya Mambo ya Katiba na Sheria.

(g) Kamati ya Mambo Mengineyo.

(h) Kamati ya kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Mashirika ya Serikali.

/51..

(2) Kwa madhumuni ya kifungu cha Katiba hii kazi na shughuli za Kamati za Baraza la Wawakilishi zitakuwa kama zitakavyoainishwa katika kanuni za Baraza la Wawakilishi.

(3) Baraza linaweza likaanzisha Kamati nyengine zo zote zinazohisi inafaa.

Baraza kutunga sheria.

86.(1) Baraza la Wawakilishi linaweza, kwa ajili ya ufanisi mzuri wa kazi zao, kutunga sheria kuhusiana na haki za wajumbe, nguvu zao, fursa na kinga zao pamoja na Kamati zao kwa misingi inayokubalika.

(2) Bila ya kuathiri masharti mengine ya Katiba hii, Baraza la Wawakilishi linaweza kufanya Kanuni za kudumu za Baraza hilo zikitilia maanani amri za kuendesha mikutano, na kwa kutilia maanani sheria zitazotungwa kwa mujibu wa kijifungu (1) cha kifungu hiki kutoka katika kanuni hizo haki za Wajumbe, nguvu zao, fursa na kinga za wajumbe wa Kamati zao.

(3) Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kutekeleza jukumu lao Barazani au kwengine kokote:-

(i) watakuwa na kinga kwa mashtaka yo yote ya jinai au hukukia.

(ii) watakuwa na kinga ya maelezo wanayoyazungumza na

(iii) hawatokamatwa wakati wakiwa katika shughuli hizo.

Lugha rasmi.

87. (1) Bila ya kuathiri kifungu hiki, lugha rasmi ya Baraza la Wawakilishi itakuwa ni Kiswahili.

(2) Kila Muswada (pamoja na vijalizo vilivyofuatana na Muswada) kila sheria inapotungwa na Baraza, kila sheria ya msingi au sheria inayopendekezwa chini ya chombo cha sheria na Baraza, maafikiano yote ya kifedha na nyaraka zenye kuhusiana na kila sheria halisi au inayopendekezwa, kusahihishwa au inayoendelea itaandikwa kwa lugha ya Kiswahili na ikihitajika kwa lugha ya Kiingereza.

Kazi za Baraza la Wawakilishi.

88.(1) Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutokana na kuwa ni Wanachama wa Chama cha Mapinduzi, wataunda kwa pamoja Kamati ya Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama ambayo kazi zake zitakua pamoja na mambo mengineyo kusimamia kwa jumla utekelezaji wa Siasa ya Chama unaofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mashirika ya Umma.

(2) Baraza la Wawakilishi pamoja na kuongoza shughuli zake kutokana na vifungu vya Katiba hii, litafanya kazi kama zilivyoelezwa kwenye kijifungu (1) kwa mambo yafuatayo ya utekelezaji:-

(a) kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitaji kuwepo kwa sheria hiyo;

(b) kujadili shughuli za kila Wizara wakati wa kikao cha mwaka cha Bajeti katika Baraza la Wawakilishi;

(c) kuuliza masuala mbali mbali kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi;

(d) kuidhinisha na kusimamia mipango ya maendeleo ya Serikali katika njia ile ile ambayo Bajeti ya mwaka inaidhinisha.

## SEHEMU YA TATU

### Kuitisha na Kuvunja Baraza la Wawakilishi

Kuitisha kikao cha Baraza la Wawakilishi.

89. (1) Bila ya kuathiri kifungu hiki kila kikao cha Baraza kitakutana sehemu yo yote katika Zanzibar na kitafanyika wakati wo wote ambapo Rais ataamuru.

(2) Kutakuwa na kikao cha Baraza la Wawakilishi angalau mara moja kila mwaka na kipindi cha miezi kumi na mbili hakitopita baina ya kikao kimoja na chengine.

Uchaguzi Mkuu na Mkutano wa Mwanzo.

90. (1) Wakati Baraza litakapovunjwa, uchaguzi Mkuu wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi utafanywa na kikao cha Baraza jipya kitafanywa si zaidi ya siku tisini toka kuvunjwa kwa Baraza lililopita.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu hiki, kikao cha Baraza la Wawakilishi katika mkutano wo wote wa Baraza kitafanyika wakati wo wote na siku yo yote kama itakavyoelezwa kulingana na Kanuni za Baraza.

kusitisha na kuvunja Baraza la Wawakilishi.

91. (1) Rais wakati wowote anaweza kusitisha Baraza la Wawakilishi kuendelea na shughuli zake.

(2) Rais anaweza wakati wo wote kulivunja Baraza la Wawakilishi.

Maisha ya Baraza la Wawakilishi.

92. (1) Maisha ya Baraza la Wawakilishi yataendelea kwa muda wa miaka mitano tangu tarehe ile ulipoitishwa Mkutano wake wa kwanza baada ya kuundwa, ila tu pale iwapo Baraza la Wawakilishi limevunjwa mapema kutokana na sababu mbali mbali zilizoelezwa katika Katiba hii.

(2) Wakati wowote Tanzania itakapokuwa iko kwenye vita, Baraza la Wawakilishi laweza mara kwa mara kuongeza kipindi cha miaka mitano iliyoelezwa katika kijifungu (1) cha kifungu hiki na si zaidi ya miezi sita kwa wakati.

## SURA YA SITA

### Sheria

### Sehemu ya Kwanza - Mahakama Kuu

Kuundwa kwa Mahkama Kuu.

93. (1)Kutakuwa na Mahkama Kuu ya Zanzibar ambayo itakuwa ndio Mahkama ya kumbukumbu na kuwa na mamlaka yote ya Kesi za Jinai na Hukukiya na nguvu nyengine zitazopewa kwa mujibu wa Katiba hii au Sheria nyengine yo yote.

(2) Majaji wa Mahkama Kuu watakuwa Jaji Mkuu na Majaji wengine, wasiopungua **wawili** wataojulikana kama Majaji wa Mahkama Kuu.

(3) Mahkama Kuu itakuwa imekamilika kisheria licha ya kuwa na nafasi wazi ya kiti cha Jaji wa Mahkama hiyo.

(4) Kazi ya Jaji haitafutwa wakati yupo mtu aliyehusika na madaraka ya kiti cha Jaji.

(5) Mahkama Kuu itakaa pahala popote ambapo Jaji Mkuu atakapoteua kwa ajili hiyo.

Uteuzi wa Majaji wa Mahkama Kuu.

94. (1) Jaji Mkuu atateuliwa na Rais.

(2) Majaji wa Mahkama Kuu watateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Tume ya uajiri ya Mahkama.

(3) Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahkama Kuu mpaka:-

(a) awe na shahada ya Sheria ya Chuo Kikuu kinachotambuliwa au Chuo cha aina hiyo; na

(b) (i) awe au amewahi kuwa Jaji wa Mahkama zilizofanana na hii kwa Kesi zote za Jinai na Hukukia katika Tanzania au sehemu yoyote ya Jumuiya ya Madola au Mahkama yenye mamlaka ya Rufaa kutoka Mahkama hizo; au

(ii) awe ni Mwanasheria wa Zanzibar au Tanzania kwa kipindi kisichopungua miaka sabab; au

(iii) awe na uzoefu, wa (i) na (ii) kwa pamoja usiopungua miaka saba.

(4) Ikitokea kwamba kiti cha Jaji Mkuu kitakuwa wazi au kwamba Jaji Mkuu atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu yoyote, basi kazi hizo zitatekelezwa na Jaji mmoja wapo atakayeteuliwa na Rais wa Zanzibar kwa ajili hiyo kama Kaimu Jaji Mkuu na Jaji huyo atatekeleza kazi hizo mpaka atakapoteuliwa Jaji Mkuu mwengine na kushika madaraka ya kiti cha Jaji Mkuu au mpaka Jaji Mkuu mwenyewe ambae alikuwa hamudu kazi zake atakaporejea kazini.

(5) Ikiwa Jaji wa Mahkama Kuu ameteuliwa kuwa Kaimu Jaji Mkuu au kwa sababu nyengine yoyote ile hawezi kufanya kazi zake za Ujaji au ikiwa Jaji Mkuu atamshauri Rais kwamba kwa hali ilivyo Mahkama Kuu inahitajia Jaji mwengine, Rais akishauriana na Tume ya uajiri ya Mahkama, anaweza kumteua mtu yeyote kuwa Jaji wa Mahkama Kuu bila ya kujali umri ulioelezewa katika kifungu 95 (1) cha Katiba hii.

(6) Mtu yeyote aliyeteuliwa chini ya kijifungu cha (5) kushikilia nafasi ya Jaji wa Mahkama Kuu, ataendelea bila kuathiri matakwa ya vifungu (4) na (6) vya kifungu 95, kushika wadhifa huo hadi hapo uteuzi wake utapofutwa na Rais kutokana na ushauri wa Tume ya uajiri ya Mahkama, na ataendelea kushikilia wadhifa huo kwa muda utaokuwa muafaka kwa kutoa hukumu au kufanya kitu chengine chochote kutokana na mambo ambayo yamefanyika mbele yake.

Muda wa kushika madaraka ya Ujaji.

95. (1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki Jaji wa Mahkama Kuu ataendelea kushika wadhifa wake hadi kufikia umri wa miaka sitini na tano.

(2) Licha ya kuwa Jaji amefikia umri uliosainishwa katika kifungu (1) hapo juu, Jaji wa Mahkama Kuu ataendelea katika wadhifa wake huo hata baada ya kufikia umri huo mpaka pale atapomaliza shughuli zote ambazo zilimfikia yeye kabla ya kutimiza umri huo.

(3) Jaji wa Mahkama Kuu ya Zanzibar aweza tu kuondolewa katika madaraka ya kazi ya Jaji kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake (ama kutokana na sababu nyengine yoyote) au kwa sababu ya tabia mbaya, na hataweza kuondolewa kazini ila kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki.

(4) Jaji wa Mahkama Kuu ataondolewa kazini na Rais ikiwa suala la kuondolewa kwake limepelekwa kwa Tume iliyoundwa kwa madhumuni hayo chini ya kifungu cha (5) cha kifungu hiki na Tume hiyo imependekeza kwa Rais kwamba Jaji huyo anafaa kuondolewa kutokana na kutomudu kazi zake au kutokana na tabia zake mbaya.

(5) Iwapo Rais anaona kwamba suala la kumuondoa Jaji Mkuu kazini linahitaji kuchunguzwa, au iwapo Jaji Mkuu atapeleka kwa Rais kwamba suala la kumuondoa Jaji linahitaji kuchunguzwa:-

(a) Rais atateua Mwenyekiti na Wajumbe wawili ambao ni Majaji au watu waliopata kuwa Majaji wa Mahkama Kuu ya Zanzibar au ya Jamhuri ya Muungano au Korti ya Rufaa ya kesi za Mahakama hizo.

(b) Tume hiyo itachunguza shauri lote halafu itatoa taarifa kwa Rais wa Zanzibar kuhusu maelezo ya shauri lote na itamshauri Rais wa Zanzibar kama huyo Jaji anayehusika aondolewe kazini kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyengine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya.

(6) Ikiwa suala la kumwondoa Jaji kazini limepelekwa kwenye Tume kwa ajili ya uchunguzi kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki Rais akishauriana na Tume ya usjiri ya Mahkama kwa suala la Jaji wa Mahkama Kuu, au kwa pendekezo lake mwenyewe kwa suala la Jaji Mkuu, anaweza kumsimamisha kazi Jaji huyo anaehusika, na kusimamishwa kazi huko kunaweza wakati wowote kutengu-liwa kwa mpango ule ule uliocelezwa wakati wa kusimamishwa kazi, na kwa vyo vyote vile uamuzi huo wa kusimamishwa kazi utakuwa hauna nguvu yoyote pale Tume itapopendekeza kwamba Jaji huyo asingestahili kuondolewa kazini.

Viapo kwa Majaji wa Mahkama Kuu.

96. Jaji wa Mahkama Kuu hatoanza kazi zake mpaka kwanza ale kiapo cha uaminifu na kiapo chingine cho chote kitachowekwa na Sheria kwa ajili hiyo.

## Sehemu ya Pili

## Mahkama ya Rufaa

Kutambuliwa kwa Mahkama ya Rufaa.

97. Kutakuwa na Mahkama ya Rufaa kwa Tanzania ambayo itakuwa Mahkama ya kumbukumbu ya kesi zote zinazopelekwa mbele yake kwa ajili ya rufaa na itakuwa na mamlaka na uwezo kwa kesi hizo kulingana na masharti yoyote yatakayoelezewa katika sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Kazi na uwezo wa Mahkama ya Rufaa.

98. (1) Uteuzi wa Majaji wa Mahkama ya Rufaa, muda wa kushika madaraka yao, nguvu, mamlaka na kazi zao zitakuwa kama zitavyo-ainishwa katika Sheria zinazohusiana na Mahkama ya Rufaa ya Tanzania.

(2) Mahkama ya Rufaa haitakuwa na uwezo wa kusikiliza kesi zozote zinazohusiana na:-

(a) Tafsiri ya Katiba hii.

(b) mambo ya Kiislam ambayo yameanzia katika Mahkama za kadhi.

(c) mambo mengine yo yote yaliyoainishwa katika Katiba hii au sheria nyengine yo yote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Sehemu ya Tatu
Mahkama Nyenginezo

Kuanzishwa kwa Mahkama Nyenginezo.

99. (1) Baraza la Wawakilishi linaweza kuanzisha Mahkama nyengine zilizo chini ya Mahkama Kuu na bila kuathiri masharti ya Katiba hii, Mahkama hizo zilizoainishwa zitakuwa na uwezo na madaraka ya aina ambayo yataainishwa katika Sheria.

(2) Mahkama Kuu itakuwa na mamlaka ya kuchunguza kesi ya aina yo yote ile, ama ya Jinai au Hukukia kutoka Mahakama za chini, na inaweza kutoa amri au maelekezo ya aina yo yote itayoona yanafaa kwa madhumuni ya kuona kwamba haki inafanyika ipasavyo.

Sehemu ya Nne
Utaratibu wa Kupeleka Hati na Kutekeleza Maagizo yaliyomo katika Hati zilizotolewa na Mahkama.

Utekelezaji wa Maagizo ya Mahkama utafanywa nchini Tanzania kote.

100.(1) Hati zenye maagizo yaliyotolewa na Mahkama za Tanzania Bara na Mahkama za Tanzania Zanzibar katika masharti ya madai ya aina zote za mashauri ya jinai ya aina zote (pamoja na hati za kuamuru kukamata watu) zaweza kupelekwa mahali popote nchini Tanzania na maagizo hayo yaweza kutekelezwa mahali popote nchini Tanzania kwa kufuata masharti yafuatayo:-

(a) iwapo Mahkama imetoa hati yenye maagizo yatakayotekelezwa mahali ambako Mahkama hiyo haina mamlaka,

basi hati hiyo itapelekwa huko na maagizo yaliyomo katika hati hiyo yatatekelezwa kwa mujibu wa utaratibu unaotumika huko kwa ajili ya kupeleka hati au kutekeleza maagizo yaliyomo katika hati iliyotolewa na Mahkama yenye mamlaka huko ilikopelekwa hati; na

(b) iwapo sheria inayotumika huko ilikopelekwa hati imeweka masharti kwamba hati zilizotolewa na Mahkama ya mahali pengine ni lazima ithibitishwe kwanza na Mahkama yenye mamlaka mahali hapo inapotumika Sheria hiyo, basi kila hati iliyotolewa na Mahkama ya mahali pengine itabidi ithibitishwe kwanza kwa mujibu wa Sheria hiyo kabla maagizo yaliyomo katika hati hiyo hayajatekelezwa.

(2) Iwapo mtu amekamatwa mahali po pote nchini Tanzania kwa mujibu wa hati ya kuamuru kukamatwa kwake iliyotolewa na Mahkama ambayo haina mamlaka mahali hapo alipokamatwa mtu huyo, basi mtu atahesabiwa kuwa yuko chini ya ulinzi halali na anaweza kufikishwa mbele ya Mahkama iliyotoa hati hiyo, lakini masharti haya yaliyomo katika kifungu hiki itabidi yatumiwe bila kuathiri masharti ya Serikali inayotumika hapo mahali alipokamatwa mtu huyo.

(3) Masharti yaliyomo katika kifungu hiki hayatazuia Sheria kuweka utaratibu kwa ajili ya kupeleka nje ya Tanzania hati zilizotolewa na Mahkama za Tanzania Bara au Mahakama za Zanzibar.

Sehemu ya Tano

Tume ya Kuajiri ya Mahakama

Tume ya Kuajiri ya Mahakama.

101. (1) Kutakuwa na Tume ya Kuajiri ya Mahkama ambayo itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(a) Jaji Mkuu kama Mwenyekiti;

(b) Mwanasheria Mkuu akiwa ni Makamo Mwenyekiti;

(c) Watu wawili ambao kwa wakati huo ni miongoni mwa Majaji wa Mahkama Kuu au Majaji wa Mahkama yo yote ya Rufaa yenye mamlaka yake Zanzibar;

(d) Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi Serikalini;na

(e) Mtu mwengine ye yote ambaye Rais ataona anafaa.

(2) Tume inaweza kufanya shughuli zake bila ya kujali nafasi iliyo wazi ya Mjumbe au kutohudhuria kwa Mjumbe yeyote, na shughuli zake hazitobatilika kwa sababu tu ya kuwepo au kujiingiza kikamilifu katika mjadala kwa mtu ambaye hahusiki.

Ila ijulikane tu kwamba uamuzi wo wote wa Tume hauna budi papatikane wingi wa kura za Wajumbe wote.

Uteuzi wa Afisa wa Mahakama.

102. (1) Uwezo wa kuwateua watu kushika nyadhifa ambazo kifungu hiki kinahusika (pamoja na uwezo wa kuwathibitisha uteuzi wao, uwezo wa kuchukua hatua za kinidhamu kwa watu wanao shikilia nyadhifa hizo na uwezo wa kuwaondowa katika nyadhifa hizo zitakuwa mikononi mwa Tume ya Uajiri ya Mahkama.

(2) Tume ya Uajiri ya Mahkama inaweza kwa maandishi, kumuagiza mtu ye yote aliyomo katika Tume hiyo au Jaji wa Mahkama Kuu au mtu ye yote anaeshikilia dhamana zilizomo chini ya kifungu hiki kufanya shughuli zake ziliopo katika kijifungu (1) cha kifungu hiki kwa masharti kama yatavyowekwa na Tume.

Ila tu pale ambapo shughuli hizo zinatakiwa ujuzi wa kisheria hazitotekelezwa na mtu mwengine ila mmoja au zaidi ya Wajumbe wa Tume ya Uajiri ya Mahkama.

(3) Afisi ambazo kifungu hiki kinahusika ni:-

(a) Afisi ya Mrajis au Naibu Mrajis wa Mahkama Kuu;

(b) Afisi ya Hakimu Mkaazi Mkuu, Hakimu Mkaazi na Hakimu wa Jimbo;

(c) Afisi ya Hakimu wa Mahkama ye yote ya chini yenye mamlaka ya kesi za Jinai;

(d) Afisi ya Kadhi;

(e) Afisi nyengine zo zote za Mjumbe wa Mahkama au zinazohusiana na Mahkama itavyoainishwa na Baraza la Wawakilishi.

## SURA YA SABA

## FEDHA

### Masharti ya Fedha yahusuyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Mfuko Mkuu wa Hazina na Fedha nyengine za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

103. (1) Kutakuwa na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao bila ya kuathiri sheria nyengine yoyote inayotumika, zitawekwa fedha zote zitakazopatikana kutokana na njia mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(2) Sheria inaweza kutungwa na Baraza la Wawakilishi kwa fedha zozote nyengine ama za kienyeji au za kigeni ambazo zitapatikana kwa matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa:-

(a) kulipwa katika mfuko wa Serikali (mbali na ule mfuko wa Hazina) na ambao utawekwa kwa shughuli maalum au

(b) kwa kuwekwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Mabenki mbali mbali ndani na nje ya nchi kwa madhumuni ya kulipia matumizi yoyote ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

ila ijulikane tu kwamba fedha hizo hazitotolewa kutoka mfuko huo mpaka iwe utolewaji wa fedha hizo umekubalika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au kwa sheria iliopitishwa na Baraza la Wawakilishi kwa madhumuni hayo.

Makadirio

104. (1) Waziri anaehusika na fedha atatayarisha makadirio ya matumizi kwa ajili ya Serikali kwa mwaka unaofuatia na atayapeleka Baraza la Wawakilishi.

/64..

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki na vifungu vinavyofuata "Matumizi yanayohitajika kisheria" maana yake ni:-

(a) matumizi yanayotoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina au katika Mapato ya Taifa kwa masharti ya vifungu vya sheria nyengine yo yote inayotumika;

(b) riba juu ya deni la Taifa, fedha zinazowekwa akiba kwa ajili ya kulipa deni, na gharama zote ambazo zinaambatana na usimamizi wa deni hilo.

Malipo ni kwa idhini ya hati maalum.

106. (1) Hakuna malipo yatayofanywa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ila kwa idhini ya Waziri anaehusika na fedha kwa kutoa waraka maalum kuhusu matumizi hayo.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu 108 hakuna idhini itayotolewa ila kwa matumizi yaliyokubaliwa na Sheria ya Matumizi ya mwaka unaohusika au kwa maelezo ya ziada au kwa kadiri itavyokuwa matumizi ya nyongeza yaliyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa kifungu 105 (2) au kwa shughuli ambazo kisheria zinalipwa toka katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

Mfuko wa matumizi ya dharura.

107. (1) Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga sheria kwa kuanzisha Mfuko wa Matumizi ya Dharura na kwa kumruhusu Waziri anaeshughulikia mambo ya fedha, ikiwa ataridhika kwamba kumekuwa na jambo la dharura na muhimu linalohitaji matumizi na ambalo hakuna njia nyengine ya kisheria ya kupata matumizi hayo, kutoa fedha katika Mfuko huo kwa ajili hiyo.

(2) Pale ambapo fedha zimetolewa katika mfuko huo, Matumizi ya Nyongeza yatapelekwa Baraza la Wawakilishi kwa haraka inavyowezekana kwa madhumuni ya kuzirejesha fedha hizo zilizotumika.

Matumizi ya Fedha kabla ya Sheria kuanza.

108. (1) Iwapo mwaka wa fedha wa Serikali umeanza na Sheria ya Matumizi ya Fedha ya Serikali inayohusika na mwaka huo haijaanza kutumika, basi Rais wa Zanzibar anaweza kuidhinisha fedha itolewe kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa ajili ya kulipia gharama za lazima za shughuli za Serikali, na fedha hizo zitatumika kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu tangu mwanzo wa mwaka wa fedha au mpaka Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali itakapoanza kutumika, kutegemea ni lipi kati ya mambo hayo litakalotokea mapema zaidi.

Kwa masharti ya kwamba uidhinishaji huo kwa kipindi hicho hautozidi robo ya fedha ambazo ziliombwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kama zilivyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa kipindi cha mwaka wa fedha uliomalizika; lakini na vile vile kwa sharti ya kwamba fedha hizo kwa pamoja zitaingizwa katika vifungu vinavyohusika katika Sheria ya Matumizi ya Fedha inayofuatia.

Deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

109.(1) Deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar litadhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(2) Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa kifungu hiki, deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar maana yake ni deni lenyewe na pia faida inayolipwa juu ya deni hilo, fedha zinazowekwa akiba kwa ajili ya kulipa deni pole pole na gharama zile zinazoambatana na usimamizi wa deni hilo.

Malipo ya kazi ya maafisa.

110. (1) Watumishi wa Serikali wanaohusika na masharti ya kifungu hiki watalipwa mshahara na posho kama itavyoelezwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(2) Mishahara na marupurupu kwa watu wanaoshika nyadhifa zinazohusiana na kifungu hiki pamoja na malipo ya uzeeni na kiinua mgongo italipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

(3) Mishahara inayolipwa kwa watu wa aina hii (mbali na posho ambalo linazingatiwa katika pencheni) hautobadilisha kwa madhumuni ya kumkandamiza baada ya kuteuliwa kwake.

(4) Inapokuwa mshahara wa mtu au masharti mengine ya utumishi yanategemea na kuchagua kwake, mshahara au masharti ambayo kwa madhumuni ya kijifungu cha (3) yatajaaliwa ni kwa manufaa yake zaidi kulikoni mshahara au masharti mengine aliyoyawacha.

(5) Kifungu hiki kinawahusu Waziri Kiongozi, Jaji Mkuu, Majaji wa Mahkama Kuu, Majaji wa Mahkama ya Rufaa, Wajumbe wa Tume ya Utumishi Serikalini, Mwanasheria Mkuu na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

111. (1) Kutakuwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar atakaeteuliwa na Rais.

(2) Mtu hatoweza kuchaguliwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mpaka awe na sifa zifuatazo:-

(a) Shahada ya Chuo Kikuu inayotambulika inayohusiana na mambo ya uchunguzi wa Hesabu au

(b) Shahada nyenginezo za diploma za uchunguzi wa hesabu na

(c) Mafunzo yanayohusiana na mambo hayo ambayo yamepatikana baada ya kupata moja kati ya shahada yo yote iliyoainishwa katika kijifungu cha (2)(a) au (b) cha kifungu hiki na kwamba amefanya kazi katika shughuli hizo kwa muda usiopungua miaka mitano.

(3) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atakuwa na jukumu juu ya mambo yafuatayo:-

(a) kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar matumizi yake yameidhinishwa kisheria na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo, basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe;

(b) kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumizi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

(c) angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahkama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoainishwa na Katiba hii na hesabu zo zote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi.

(4) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na kila mtumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar aliyeruhusiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atakuwa na haki ya kuchunguza vitabu kumbukumbu, hati za maelezo, taarifa na hati nyenginezo zote zinazohusika na hesabu za aina yo yote iliyotajwa katika kijifungu (3) cha kifungu hiki.

(5) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atawasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa kwa mujibu wa masharti ya kijifungu (3) (c) cha kifungu hiki. Baada ya kupokea taarifa hiyo Rais atamwagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Baraza la Wawakilishi kitachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza kikao hicho. Iwapo Rais hatachukua hatua za kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Baraza la Wawakilishi, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi au Naibu Spika ambae atawasilisha taarifa hiyo kwenye Baraza la Wawakilishi.

(6) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atakuwa pia na jukumu la kutekeleza kazi za shughuli nyingine, na atakuwa na madaraka mengine ya namna mbali mbali, kama itakavyoelezwa na sheria, kuhusu hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au hesabu za Mashirika na Makampuni ya Umma ya Zanzibar.

/70...

(7) Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya kijifungu (3), (4) na (5) ya kifungu hiki, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu hatalazimika kufuata amri ya maagizo ya mtu mwengine ye yote au ya Idara yo yote ya Serikali, lakini maelezo haya ya kifungu hiki hayataizuia Mahkama nayo kutumia madaraka yake kwa ajili ya kuchunguza kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ametekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au sivyo.

(8) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hatoanza kazi yake ila kwanza ale kiapo cha uaminifu na kiapo chengine cho chote kitachowekwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya utendaji wake wa kazi.

Kumuondoa kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

112. (1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anaweza tu kuondolewa katika madaraka ya kazi yake kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake (ama kutokana na maradhi au sababu nyengine yo yote) au kwa sababu ya tabia mbaya, na hataweza kuondolewa kazini ila kwa mujibu wa masharti ya kijifungu (3) cha kifungu hiki. Vinginevyo ataendelea na kazi hiyo hadi kutimiza umri wa kuacha kazi kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(2) Iwapo suala la kumwondoa kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki linahitaji kuchunguzwa, basi utaratibu ufuatao ndio utakaotumika:-

(a) Rais atateua Tume Maalum ambayo itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiopungua wawili;

(b) Tume hiyo itachunguza shauri lote halafu itatoa taarifa kwa Rais kuhusu maelezo ya shauri lote pamoja na ushauri wao kama huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu aondolewe kazini kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyengine yo yote au kwa sababu ya tabia mbaya.

(3) Ikiwa Tume iliyoteuliwa kwa mujibu wa masharti ya kijifungu (2) itamshauri Rais kwamba huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu aondolewe kazini kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyengine yo yote au kwa sababu ya tabia mbaya, basi Rais atamuondoa kazini.

(4) Iwapo Tume itamshauri Rais kwamba huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu asiondolewe kazini basi Rais anaweza kukubali au kukataa mapendekezo hayo na hapo Rais atatumia busara zake.

(5) Mtu ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu au aliyepata kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu hawezi kuteuliwa kushika au kushikilia madaraka ya kazi nyengine yoyote katika utumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## Sehemu ya Pili

## Masharti ya Fedha yahusuyo mambo ya Muungano

Mchango wa Muungano.

113. (1) Fedha zote ambazo ni sehemu ya mchango wa Muungano na ambazo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinawajibika kulipa zitakuwa ni gharama itayotoka kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

Uwezo wa kutumia Kasma.

114. Hakuna fedha itayotumiwa katika sehemu hii mpaka baada ya:-

(a) Tume ya pamoja ya fedha inayohusu mambo ya Muungano kama ilivyoanzishwa na Katiba ya Muungano imechambua mapato na matumizi ya shughuli za Muungano na kutoa mapendekezo yake kwa vyombo vinavyohusika juu ya mgawanyo wa matumizi hayo; na

(b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuyakubali mapendekezo hayo na mgawanyo wake.

## SURA YA NANE

### Tume ya Utumishi Serikalini

Tume ya Utumishi.

115. (1) Kutakuwa na Tume ya Utumishi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itayokuwa na Mwenyekiti, Makamo Mwenyekiti na Wajumbe wengine watano.

(2) Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume watateuliwa na Rais.

Uteuzi na kumalizika kwa ujumbe wa Mjumbe.

116. (1) Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume ya Utumishi Serikalini ikiwa:-

(a) ni Waziri; au ni mjumbe wa Baraza la Mapinduzi;

(b) ni Naibu Waziri; au

(c) ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi; au

(d) anashika wadhifa wo wote katika Chama cha Mapinduzi au Jumuiya zake; au

(e) ni mfanyakazi Serikalini.

(2) Kiti cha Mjumbe wa Tume kitakuwa wazi:-

(a) baada ya kumalizika miaka mitatu kuanzia siku ambayo mjumbe anaeshikilia kiti hicho aliteuliwa; au

(b) ikiwa kumetokea jambo lo lote ambalo kama mtu anaeshikilia kiti kimoja wapo si Mjumbe basi asingelifaa kuwa Mjumbe wa Tume.

Ila ijulikane kwamba Mjumbe huyo anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine cha miaka mitatu na si zaidi.

(3) Mjumbe wa Tume anaweza kuondolewa katika kiti chake kutokana na kutokumudu kwake kazi alizokabidhiwa (ama kwa ajili ya maradhi ya mwili au akili au kwa sababu nyengine yo yote ile) au kwa utovu wa nidhamu, na hatoweza kuondolewa ila kwa kufuata masharti ya kifungu hiki.

(4) Mjumbe wa Tume ataondolewa kwenye madaraka yake na Rais ikiwa suala la kuondolewa kwake kwenye madaraka limepelekwa kwa Tume Maalum iliyoundwa kwa ajili hiyo chini ya kijifungu cha (5) na Tume hiyo imependekeza kwa Rais kwamba mjumbe huyo angefaa aondolewe kutokana na kutomudu kazi zake kama ilivyoelezwa hapo juu.

(5) Ikiwa Rais atahisi kwamba suala la kumuondoa Mjumbe wa Tume lingefaa kuchunguzwa basi:-

(a) Rais atateua Tume Maalum itayokuwa na Mwenyekiti na wajumbe wasiopungua wawili kutokana na watu wanaoshikilia au waliowahi kushika wadhifa wa Jaji wa Mahkama zenye mamlaka kusikiliza kesi za aina zote Tanzania au Jaji wa Mahkama ya Rufaa yenye mamlaka ya rufaa kutoka Mahkama hizo; na

(b) Tume itachunguza suala hilo na itapendekeza kwa Rais kama Mjumbe huyo anafaa aondolewe au laa.

(6) Ikiwa suala la kumwondoa mjumbe limepelekwa kwa Tume Maalum kwa kuchunguzwa, Rais anaweza kumsimamisha kazi Mjumbe huyo na kusimamishwa huko kunaweza wakati wo wote kukatenguliwa na Rais, na kwa hali yoyote hakutakuwa na taathira yoyote ikiwa Tume hiyo imependekeza kwamba mjumbe huyo asiondolewe kwenye madaraka yake.

(7) Ikiwa kiti cha Mwenyekiti wa Tume kiwazi, au iwapo Mwenyekiti, kutokana na sababu yo yote ile hawezi kutekeleza kazi zake, basi hadi hapo mtu atakaeteuliwa kushika, na kuwa ameshaanza kushika kazi za Mwenyekiti, au hadi hapo Mwenyekiti atapomudu kufanya kazi zake kwa kadiri itavyokuwa, Naibu Mwenyekiti, au ikiwa kiti cha Naibu Mwenyekiti kiwazi, au ikiwa Naibu Mwenyekiti kwa sababu zozote zile hawezi kutekeleza kazi za Mwenyekiti, mjumbe mwengine yo yote atayeteuliwa na Rais; atashikilia madaraka ya Mwenyekiti na Naibu Mwenyekiti au mjumbe mwengine ataendelea kushikilia madaraka hayo, bila ya kuathiri masharti ya vijifungu vya (2), (4) na (5), kwa kadiri itavyokuwa hadi hapo Mwenyekiti ataporejea katika kazi zake hizo.

(8) Ikiwa kiti cha mjumbe wa Tume mbali na kile cha Mwenyekiti kiwazi, au ikiwa mjumbe huyo anashikilia nafasi ya Mwenyekiti chini ya kijifungu cha (7) au kwa sababu nyengine yo yote hawezi kumudu kazi zake, Rais anaweza kumteua mtu anaofaa kushikilia nafasi ya mjumbe huyo na mtu huyo aliyeteuliwa ataendelea na kazi hiyo bila ya kuathiri masharti ya vijifungu (2), (4) na (5) hadi hapo Mjumbe mwenyewe ataporejea katika kazi žake.

(9) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii, Tume katika kutekeleza majukumu yake haitowajibika kuchukua amri au maelekezo ya mtu ye yote yule.

(10) Tume, kwa kuzingatia kanuni zake, inaweza kufanya kazi licha ya kutokuhudhuria au kuwepo wazi kwa kiti cha mjumbe, na shughuli zake hazitobatilishwa kwa sababu ya kuwepo mtu mwengine asiyehusika.

Isipokuwa kwamba uamuzi wowote ule wa Tume itabidi upate wingi wa kura zisizopungua thuluthi mbili ya wajumbe wote.

Uteuzi wa wafanyakazi wa Serikali.

117. (1) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii, uwezo wa kuteua watu kushika nafasi za kazi Serikalini (pamoja na uwezo wa kuwahakikisha kazini mwao), uwezo wa kutoa adhabu kwa watovu wa nidhamu katika nyadhifa hizo na uwezo wa kuwaondoa katika madaraka hayo utakuwa katika Tume ya Utumishi ya Zanzibar.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki pamoja na kijifungu cha (9) cha kifungu 116 sheria inaweza kutungwa na Baraza la Wawakilishi ikiwa kuweka utaratibu wa kufanya kazi za Tume chini ya kifungu hichi na mambo mengine yote yanayohusiana na shughuli hizo.

(3) Hakuna mtu atayeteuliwa chini ya kifungu hiki kwa kufanya kazi yo yote katika Afisi ya Rais bila ya kupata kibali cha Rais.

(4) Kijifungu cha (1) hakitohusika na uteuzi wa watu katika Afisi zifuatazo:-

(a) afisi za Wawakilishi wakuu wa Zanzibar katika nchi nyengine yo yote, na

(b) afisi yo yote katika shughuli za Serikali ambazo uteuzi wake umeelezewa kisheria.

## SURA YA TISA

### Tume ya Uchaguzi

Tume ya Uchaguzi.

118. (1) Kutakuwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo itakuwa na Spika wa Baraza la Wawakilishi akiwa Mwenyekiti na si zaidi ya Wajumbe wengine watano watakaoteuliwa na Rais.

(2) Tume itateua Makamo Mwenyekiti wake kutoka miongoni mwa wajumbe wengine.

(3) Hakuna mtu atakayeteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume akiwa ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au akiwa ni miongoni mwa majeshi ya Tanzania, au ana wadhifa wo wote ambao kisheria hahusiki kuwa Mjumbe wa Tume.

(4) Bila ya kuathiri masharti mengine ya kifungu hiki kiti cha Mjumbe wa Tume kitakuwa wazi:-

(a) baada ya kupita miaka mitano tokea siku aliyoanza kuteuliwa;

(b) baada ya kutokea jambo lo lote au kitu chochote ambacho kama si mjumbe kingemfanya asiweze kuwa Mjumbe wa Tume hiyo.

(5) Mjumbe wa Tume anaweza kuondolewa tu kutokana na kutokumudu kazi zake (iwe kutokana na ugonjwa wa mwili au kiakili au kutokana na sababu nyengine yo yote ile) au kwa utovu wa nidhamu na hataondoshwa madarakani humo ila kwa kufuata masharti ya kifungu hiki.

(6) Mjumbe wa Tume ataondolewa kwenye madaraka yake na Rais ikiwa suala la kuondolewa kwake kwenye madaraka limepelekwa kwa Tume Maalum iliyoundwa kwa ajili hiyo chini ya kijifungu cha (7) na Tume hiyo imependekeza kwa Rais kwamba mjumbe huyo angefaa aondolewe kutokana na kutomudu kazi zake kama ilivyoelezwa hapo juu.

(7) Ikiwa Rais atahisi kwamba suala la kumwondoa Mjumbe wa Tume lingefaa kuchunguzwa, basi:-

(a) Rais atateua Tume Maalum itayokuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wasiopungua wawili kutokana na watu wanaoshikilia au waliowahi kushika wadhifa wa Jaji wa Mahkama zenye mamlaka ya kusikiliza kesi za aina zote Tanzania, au Jaji wa Mahkama ya Rufaa yenye mamlaka ya rufaa kutoka Mahkama hizo; na

(b) Tume itachunguza suala hilo na litapendekeza kwa Rais kama Mjumbe huyo angefaa aondolewe au la.

(8) Ikiwa suala la kumwondoa Mjumbe limepelekwa kwa Tume Maalum kwa kuchunguzwa, Rais anaweza kumsimamisha kazi mjumbe huyo na kumsimamisha huko kunaweza wakati wowote kukatenguliwa na Rais, na kwa hali yoyote hakutokuwa na taathira yo yote ikiwa Tume hiyo imependekeza kwamba mjumbe huyo asiondolewe kwenye madaraka yake.

(9) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii, Tume katika kutekeleza majukumu yake haitowajibika kuchukua amri au maelekezo ya mtu yo yote yule.

(10) Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga Sheria ya uteuzi utaofanywa na Tume ya Uchaguzi wa Wajumbe kwa kushughulikia uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani; na bila ya kuathiri masharti ya sheria hiyo, au maelekezo ya Tume ya Uchaguzi, Wajumbe hao wanaweza kutumia uwezo wa Tume ya Uchaguzi kwa ajili ya kushughulikia Uchaguzi huo.

(11) Hakuna Mahkama yo yote itayoingilia suala lolote litalofanywa na Tume ya Uchaguzi katika kazi zake chini ya sura hii.

Ila ijulikane kwamba, kitu hicho, kilichofanywa au kitakachofanywa kinathibitishwa na Mwenyekiti wa Tume kwa maandishi yake kwamba ni kwa mujibu wa uwezo wao na ni katika kutekeleza kazi zao kwa mujibu wa matakwa ya sura hii.

(12) Tume, kwa kuzingatia kanuni zake, inaweza kufanya kazi licha ya kutokuhudhuria au kuwepo wazi kwa kiti cha mjumbe, na shughuli zake hazitobadilishwa kwa sababu ya kuwepo mtu mwengine asiyehusika.

Isipokuwa kwamba uamuzi wo wote ule wa Tume itabidi upate wingi wa kura za wajumbe wote.

Majimbo.

119. (1) Bila kuathiri masharti ya kifungu hiki, Zanzibar inaweza kugaiwa katika majimbo ya uchaguzi yenye majina na mipaka kama yatavyoelezwa na Tume.

(2) Baraza la Wawakilishi linaweza kuweka kisheria, idadi ndogo kabisa ya majimbo ya uchaguzi yasiyopungua 40 na idadi kubwa kabisa ya majimbo yasiyozidi 55.

(3) Majimbo yote yatakuwa karibu na wakaazi sawa sawa kama itakavyoonekana na Tume, lakini Tume inaweza kuiepuka shuruti hii kwa kiwango kile kinachofikiria kuwa inafaa kwa ajili ya kuzingatia:-

(a) Idadi ya watu, na zaidi katika kuhakikisha uwakilishi unaofaa katika miji mikubwa na miji ya mashamba yenye idadi ndogo ya watu;

(b) ukuaji wa idadi ya watu;

(c) njia za usafiri;

(d) maumbile ya kijografia yaliopo katika jimbo hilo; na

(e) mipaka ya sehemu za utawala, na kwa madhumuni ya kifungu hiki idadi ya wakaazi wa sehemu yo yote ya Zanzibar itahakikishwa na ripoti ya kuhesabu watu ya karibuni sana ambayo imefanywa kwa mujibu wa sheria.

(4) Katika kipindi cha miaka 8 hadi 10 au wakati wo wote Baraza la Wawakilishi litakapoamuru kufanywa hivyo Tume itachunguza idadi ya mipaka na majina ya majimbo hayo kwa kiwango kile ambacho inahisi ni wajibu kuangaliwa upya; na inaweza kwa kutoa tangazo, kubadili idadi, mipaka na majina ya majimbo hayo.

(5) Iwapo hesabu ya idadi ya watu imeshafanywa kwa mujibu wa sheria, au iwapo mabadiliko yamefanywa katika mipaka ya sehemu yo yote ya utawala, Tume inaweza ikachunguza suala hilo na kuweka mabadiliko hayo katika kiwango kile ambacho Tume inahisi ingefaa kufanyiwa mabadiliko hayo.

/80..

(6) Amri yo yote iliyofanywa na Tume chini ya kifungu hiki itatangazwa katika Gazeti na itaanza kutumika tarehe ambayo itaainishwa katika Gazeti hilo.

SURA YA KUMI

Idara Maalum

Idara Maalum.

120. (1) Kutakuwa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo kazi zake na shughuli zake zitakuwa kama zitavyoainishwa katika sheria zinazohusika.

(2) Idara Maalum zilizoainishwa katika kijifungu (1) hapo juu ni:-

(a) Jeshi la Kujenga Uchumi (kwa ufupi J.K.U.);

(b) Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (kwa ufupi KMKM); na

(c) Chuo cha Mafunzo (cha wahalifu).

(3) Rais wa Zanzibar anaweza, ikiwa ataona inafaa kuanzisha Idara nyengine yo yote kuwa Idara Maalum.

Tume ya Uajiri ya Idara Maalum.

121. (1) Kutakuwa na Tume ya uajiri ya Idara Maalum ambayo uwezo wake, nguvu zake, kazi zake na kanuni za mwenendo wake zitakuwa kama zitavyoainishwa katika Sheria itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili hiyo.

Uwezo wa Rais katika Idara Maalum.

122. (1) Rais atakuwa Kamanda Mkuu wa Idara Maalum na atakuwa na uwezo wa kufanya chochote kile anachohisi, kwa maslahi ya Taifa, kinafaa.

(2) Uwezo wa Rais chini ya kijifungu (1) unaingiza uwezo wa kutoa amri ya kufanya shughuli yo yote inayohusiana na Idara hiyo kwa manufaa ya Taifa.

/81..

SURA YA KUMI NA MOJA
Mamlaka ya Baadhi ya Vyombo vya Muungano

Mahkama ya Katiba, Tume ya kudumu ya Uchunguzi Tume ya Tabia za Viongozi na Tume ya Uchaguzi kutumika Zanzibar.

123. (1) Vyombo vilivyoainishwa chini ya kifungu (2), cha kifungu hichi na kama vilivyoanzishwa kwa mujibu wa vifungu vya Katiba ya Muungano, vitakuwa na mamlaka ya kutekeleza shughuli zake Zanzibar kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa katika Katiba ya Muungano na Sheria yo yote nyengine iliyoundwa na ama Bunge au Baraza la Wawakilishi kwa ajili hiyo.

(2) Vyombo vyenyewe vilivyotajwa katika kijifungu (1) ni:-

(a) Mahkama ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano

(b) Tume ya Kudumu ya Uchunguzi;

(c) Tume ya Tabia za Viongozi; na

(d) Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, vyombo vilivyoainishwa katika kijifungu cha (2) vitahesabika kama ni vyombo vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika shughuli zake hapa Zanzibar.

SURA YA KUMI NA MBILI
Vyombo vyengine vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
Sehemu ya Kwanza
Baraza la Mipango na Tume ya Kudumu ya Mipango

Baraza la Mipango.

124. Kutakuwa na Baraza la Mipango katika Serikali ya Zanzibar ambalo ndiyo chombo kikuu kinachoandaa na kusimamia utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii kwa upande wa Zanzibar.

Wajumbe wa Baraza.

125. Wajumbe wa Baraza la Mipango pamoja na utaratibu wa Mikutano utakuwa kwa mujibu wa sheria itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Tume ya Kudumu ya Mipango.

126. (1) Kutakuwa na Tume ya Kudumu ya Baraza la Mipango Zanzibar ambayo itakuwa ni chombo cha utekelezaji cha Baraza la Mipango.

(2) Utaratibu wa kutekeleza shughuli za Tume pamoja na muundo wake utakuwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi au sheria nyingine inayohusika Zanzibar.

(3) Kutakuwa na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango atakaeteuliwa na Rais.

## Sehemu ya Pili

## Serikali za Mitaa

Serikali za Mitaa.

127. Kutakuwa na Serikali za Mitaa kwa kila Mkoa, Wilaya na Eneo kwa ajili ya Mkoa huo au Wilaya hiyo au Eneo hilo kwa kadiri itavyokuwa.

(2) Uteuzi wa Wajumbe, madaraka na kazi ya kila Serikali ya Mtaa zitakuwa kama zitavyoainishwa na sheria iliotungwa na Baraza la Wawakilishi.

## SURA YA KUMI NA TATU

### Mambo ya Jumla

Kujiuzulu.

128. (1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, mtu ye yote ambae ametajwa, amechaguliwa au ameteuliwa kushika wadhifa wo wote ule ulioainishwa na Katiba hii, anaweza kujiuzulu kutoka katika wadhifa huo kwa maandishi ya mkono wake akiyapeleka kwa mtu aliyemtaja, aliyemchagua au aliyemteua.

(2) Mtu aliyetoa taarifa ya kujiuzulu kwa mujibu wa masharti ya kijifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, atahesabiwa kuwa amejiuzulu tangu siku ile ambayo taarifa yake ya kujiuzulu itakapopokelewa na mtu yeyote aliyeruhusiwa kuipokea taarifa hiyo na mtu anayehusika na kikao kinachohusika, lakini kama taarifa hiyo ya kujiuzulu imeeleza kwamba mtu huyo atahesabiwa kuwa amejiuzulu tangu siku hiyo nyingine ya baadae.

(3) Taarifa ya kujiuzulu kwa Rais itapelekwa kwa Halmashauri Kuu ya Taifa.

(4) Taarifa ya kujiuzulu kwa Waziri Kiongozi itapelekwa kwa Rais.

(5) Taarifa ya kujiuzulu kwa Spika, au Naibu Spika, wa Baraza la Wawakilishi itapelekwa kwa Baraza la Wawakilishi.

(6) Taarifa ya kujiuzulu kwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au kutoka kwa Mwenyekiti na Mjumbe wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi itapelekwa kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi.

Uteuzi mpya na wa kuarifiwa kwa kuachishwa kazi.

129. (1) Iwapo mtu ye yote mwenye dhamana ya kazi ye yote iliyoanzishwa na Katiba hii amejiuzulu, basi ikiwa anazo sifa zote zinazohitajika na kwa kila hali anastahili, anaweza kuteuliwa kuchaguliwa tena kushika madaraka ya kazi hiyo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(2) Iwapo mtu ameachishwa kazi au amesimamishwa kazi itabidi chombo hicho au mtu huyo aliemuachisha au aliemsimamisha kazi amueleze kwa maandishi kwamba amemuachisha au amemsimamisha kazi.

Maelezo kuhusu utaratibu wa kukabidhi madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali.

130. (1) Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya Katiba hii kuhusu utaratibu wa kukabidhi madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ifahamike kuwa mtu ye yote mwenye mamlaka kwa mujibu wa Katiba hii, ya kumteua au kuchagua mtu mwingine kushika madaraka ya kazi fulani anao pia uwezo wa kumteua au kumchagua Naibu au mtu ambaye atashika kwa muda na kutekeleza madaraka ya kazi hiyo.

Sheria za Muungano.

131. (1) Hakuna sheria yo yote itakayopitishwa na Bunge la Muungano ambayo itatumika Zanzibar mpaka sheria hiyo iwe ni kwa ajili ya mambo ya Muungano tu na ipitishwe kulingana na maelekezo yaliyo chini ya vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

(2) Sheria kama hiyo lazima ipelekwe mbele ya Baraza la Wawakilishi na Waziri anayehusika.

(3) Pale sheria ndogo inapoundwa kwa mujibu wa uwezo uliowekwa chini ya kifungu cha (1) na (2) cha sheria hii itatumika tu pale itakapotimiza shuruti zote zilizowekwa kwa matumizi ya sheria mama kama ilivyoainishwa katika kifungu hiki.

Masharti ya kutoza kodi.

132. Hakuna kodi ya aina yo yote itakayotozwa isipokuwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi au kwa utaratibu uliowekwa kisheria na uliotiliwa nguvu ya kisheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(2) Masharti yaliyomo katika kijifungu (1) cha kifungu hichi hayatalizuia Bunge kutumia mamlaka yake ya kutoza kodi ya aina yo yote inayohusiana na mambo ya Muungano kwa mujibu wa madaraka ya Bunge hilo.

Kwa kujua kwamba mashauriano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano yamefanywa na kukubalika sehemu zote mbili kabla kupitishwa sheria.

Ufafanuzi.

133. (1) Katika Katiba hii, ila iwapo maelezo yanahitaji vyenginevyo:-

"Baraza la Mapinduzi" linajumuisha na Baraza la Mawaziri;

"Chama" maana yake ni Chama cha Mapinduzi (CCM);

"kiapo" kinajumuisha na uthibitisho;

"Kiapo cha uaminifu" ina maana ya kiapo chochote cha uaminifu kama kitavyoainishwa na Baraza la Wawakilishi;

"Mfanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar" maana yake ni mtu anaefanyakazi au anaeshikilia wadhifa wa kazi katika utumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na mashirika yake;

"Mwaka wa fedha" maana yake ni kipindi cha miezi 12 kinachomalizikia tarehe 30 Juni ya mwaka wowote au kwa siku nyingine yoyote kama Baraza la Wawakilishi litavyoainisha kwenye sheria.

"Rais" ina maana ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Waziri" maana yake ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Memba wa Baraza la Mapinduzi aliyekabidhiwa wadhifa wa kazi ya Waziri katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(2) Ila iwapo maelezo yahitaji vyenginevyo, uwezo wo wote uliopewa Baraza la Wawakilishi na Katiba hii kwa kuanzisha, au kuelezea jambo lo lote basi utafanywa kwa kuandikwa Sheria;

(3) Kwa madhumuni ya Katiba hii, mtu hatahesabiwa kuwa ana madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sababu tu kwamba anapokea malipo ya uzeeni au malipo mengine ya aina hiyo kwa ajili ya utumishi wake wa zamani.

(4) Katika Katiba hii, ila iwapo maelezo yahitaji vingine, kila anapotajwa mtu mwenye dhamana ya kazi fulani kwa kutaja madaraka ya kazi yake, ifahamike kuwa mtu anayehusika kuwa ni pamoja na mtu ye yote ambaye ni Kaimu au aliyeteuliwa kwa njia ya halali kushikilia dhamana ya kazi hiyo.

(5) Iwapo Katiba inatoa uwezo au nguvu fulani, basi uwezo huo au nguvu hizo zinaweza kutekelezwa wakati wo wote inapohitajika.

(6) Katika Katiba hii, kila yalipotajwa mamlaka ya kumwondoa mtu katika madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ifahamike kuwa mamlaka yanayohusika ni pamoja na mamlaka yaliyotolewa kwa mujibu wa masharti ya sheria yo yote yanayomtaka mtu huyo au yanayomruhusu mtu huyo kustaafu.

(7) Iwapo mtu ameteuliwa, kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, kuwa Naibu au kushikilia madaraka ya kazi fulani wakati mtu maalum aliyeteuliwa kushika madaraka ya kazi hiyo anashindwa kutekeleza shughuli zinazohusika na kazi hiyo, basi haitaruhusiwa kufanya uchunguzi wo wote au kutoa hoja yo yote juu ya uteuzi wa huyo Naibu eti kwa sababu kwamba huyo mtu maalum aliyeteuliwa kushika madaraka ya kazi hiyo hakushindwa kutekeleza shughuli zinazohusika na kazi hiyo.

(8) Katika kifungu cho chote cha Katiba hii kinachosema kwamba hakuna mtu au chombo fulani kitachoingilia mtu au chombo cho chote katika kutekeleza kazi zake basi hakitokuwa na maana ya kwamba Mahkama zitazuilika katika mamlaka yake katika suala lo lote hata kama mtu huyo au chombo hicho kimetekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba hii au sheria nyengine yo yote.

(9) Katika Katiba hii, kila ilipotajwa sheria ambayo inabadilisha au kufuata sheria nyengine, ifahamike kuwa sheria inayohusika ni pamoja na sheria ambayo inarekebisha sheria hiyo nyingine au ambayo inaendelea kutumika kwa hiyo sheria nyingine, ama bila mabadiliko au baada ya kubadilishwa au kurekebishwa, au sheria ambayo inaweka masharti mapya katika sheria nyingine.

Jina la Katiba na tarehe ya kuanza kutumika.

134. (1) Jina la Katiba hii litakuwa "Katiba ya Zanzibar".

(2) Katiba hii itaanza kutumika tarehe ambayo itatangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

IMEPITISHWA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI
TAREHE 10 OKTOBA, 1984.

IDI PANDU HASSAN
KATIBU
BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR.

SHERIA YA KATIBA (MASHARTI YA MUDA)
YA 1984

SEHEMU.

1. Jina fupi, tarehe ya kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.
3. Sheria hii kuwa na nguvu juu ya Katiba.
4. Uendelezwaji sheria wa sheria zilizopita.
5. Mahitajio ya Katiba kutimizwa kwa sheria zilizopo.
6. Mambo yaliyobakia.
7. Maofisi na Maofisa.
8. Kuendelea kwa Baraza la Wawakilishi lililoanzishwa chini ya Katiba ya 1979.
9. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Memba wa Baraza la Mapinduzi.
10. Kuendelezwa ka mashauri Mahkamani.
11. Kufutwa kwa Katiba ya 1979 na mambo ya muda na kuhalalisha baadhi ya mambo.
12. Tarehe ya kutangazwa kwa Katiba.

<u>SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR</u>

NAMBA 6 YA 1984

NAKUBALI

ALI HASSAN MWINYI
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI

1 - 12 - 1984.

**SHERIA YA KUWEKA MASHARTI YA KUHALALISHA BAADHI YA MAMBO KUTOKANA NA KUPITISHWA KWA KATIBA YA ZANZIBAR YA 1984 NA MAMBO YANAYOHUSIANA NA UWEKAJI WA KATIBA HIYO**

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Jina fupi, tarehe ya kuanza kutumika.

1. Sheria hii inaweza kuitwa Sheria ya Katiba (masharti ya muda) ya 1984, na itasomwa pamoja na Katiba ya Zanzibar ya 1984, na itaanza kutumika tarehe itakayoanza kutumika Katiba hiyo.

Ufafanuzi.

2. Katika Sheria hii, ila iwapo itaelezwa vyenginevyo:-

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, ambayo imepitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

"Sheria iliyokuwepo" maana yake ni sheria kama ilivyokuwa mara tu kabla ya utumikaji wa Katiba, na kwa kutoa wasiwasi wo wote ule inajumuisha sheria iliyotungwa kabla ya kutumika au baada ya kutumika kwa Katiba hii.

"Katiba ya 1979" maana yake ni Katiba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya mwaka 1979.

Sheria hii kuwa na nguvu juu ya Katiba.

3. Vifungu vya Sheria hii vitatumika bila ya kujali masharti yo yote yaliyomo ndani ya Katiba.

Uendelezwaji sheria wa sheria zilizopita.

4. (1) Bila ya kuathiri urekebishwaji, ufutwaji au ubadilishwaji wa sheria yo yote iliyokuwepo, kuanzia tarehe ya kutumika kwa Katiba hii, sheria zilizopo, zitaendelea kuwa sheria za Zanzibar baada ya kuanza kutumika Katiba ila tu pale sheria yenyewe inaporekebishwa, inapobadilishwa au inapofutwa na chombo kinachohusika au pale ambapo kifungu cho chote kinamalizika matumizi yake baada ya kuanza kutumika kwa Katiba.

(2) Sheria ziliopo zitafafanuliwa pamoja na mabadiliko, maingizo, matengenezo au makatazo ambayo ni lazima yafanywe ili kuhakikisha matakwa ya Katiba hii, na kwa kuondoa wasiwasi wo wote ule hapa inaelezwa kwamba bila ya kuathiri mabadiliko hayo, maingizo, matengenezo au makatazo yo yote ambayo sheria hiyo imefanyiwa, na vile vile bila ya kuathiri vifungu vyengine vya sheria hii, matumizi ya Sheria zilizopo baada ya kuanza kutumika kwa Katiba hii hayatoathirika kwa sababu ya kufutwa kwa Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya 1979.

(3) Rais anaweza, wakati wo wote kabla ya tarehe 31 Machi, 1985, kwa agizo litakalochapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali kufanya marekebisho ya sheria yo yote iliyopo ambayo ataona inafaa na ni muhimu ili kuiweka sheria hiyo katika matakwa ya Katiba hii au kwa kutilia nguvu katika vifungu vya Katiba hii.

Mahitajio ya Katiba kutimizwa kwa sheria zilizopo.

5. Pale ambapo kitu cho chote kilichoelezewa ndani ya Katiba kinahitajiwa kifanyiwe sheria na Baraza la Wawakilishi au chombo chengine cho chote kimetekelezwa chini ya sheria zilizopo (pamoja na mabadiliko yo yote kama ilivyoelezwa chini ya kifungu cha 4 cha sheria hii utekelezwaji huo utakuwa halali kama kwamba umefanywa chini ya Katiba na kufanywa sheria na Baraza la Wawakilishi au chombo chengine cho chote kinachohusika, kwa kadiri itavyokuwa.

Mambo yaliyobakia.

6. Pale jambo lo lote au kitu cho chote kitakapokuwa kimeshaanza kutumika, au hatua imechukuliwa kabla ya kuanza kutumika kwa sheria hii na mtu ye yote au chombo cho chote

chenye uwezo wa kisheria zilizopo, jambo hilo au kitu hicho kinaweza kuendelezwa na kumalizwa na hatua nyengine zo zote zinaweza kuchukuliwa na mtu huyo au chombo hicho kilicho na uwezo kisheria wakati au baada ya kutumika kwa sheria hii na haitokuwa lazima kwa mtu mwengine au chombo chengine kulipitia upya au kuanza tena upya kitu hicho au jambo hilo.

Maofisi na Maofisa.

7. (1) Bila ya kuathiri masharti ya kijifungu cha (2) na cha (3) cha kifungu hichi, kila mtu ambaye, kabla ya kuanza kutumika Katiba, ana wadhifa, au anashikilia wadhifa wo wote ulioanzishwa chini ya Katiba ya 1979, kwa pale ambapo haiathiri Katiba, atajaaliwa tokea kuanza kwa Katiba, kuwa ameteuliwa au kuchaguliwa katika ofisi hiyo au kushikilia wadhifa huo kama ulivyoanzishwa na Katiba na atajaaliwa kuwa katika utumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwamba ametimiza matakwa yote ya Katiba au sheria nyengine, kwamba amekula kiapo cha uaminifu kinachohitajika katika kuchaguliwa au kuteuliwa katika wadhifa huo.

(2) Mtu ye yote ambae kwa mujibu wa Katiba ya 1979, anatakiwa aondoke katika wadhifa wake baada ya kufikia umri fulani au baada ya kumalizika muda fulani basi ataondoka katika wadhifa huo baada ya kufikia umri au muda uliowekwa kwa wadhifa huo kwa mujibu wa Katiba.

(3) Matakwa ya kifungu hichi yatatumika bila ya kuathiri uwezo uliowekwa na Katiba kwa mtu yo yote yule wa kuanzisha, katika ofisi fulani, kumuondoa mtu katika wadhifa fulani au kumtaka mtu astaafu kutoka wadhifa fulani.

Kuendelea kwa Baraza la Wawakilishi lililoanzishwa chini ya Katiba ya 1979.

8. (1) Bila ya kuathiri kifungu cha (2) cha kifungu hichi, lakini pia bila ya kujali, kuanzishwa kwa Katiba hiyo kuhusiana na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Spika na watu wengine ambao kabla ya kuanza kwa Katiba, walikuwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Katiba ya 1979, wataendelea kuwa Spika na Wajumbe wa, na watafanya Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Katiba hadi hapo Baraza litakapovunjwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba.

(2) Kijifungu cha (1) cha kifungu hichi kitatumika bila ya kuathiri matumizi ya vifungu vya Katiba ya 1979, vinavyohusika na nafasi ya Spika kuwa wazi au nafasi ya mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwa wazi katika masingira yale yale yaliyoelezewa na Katiba ya 1979.

(3) Kanuni za Baraza na amri ya kanuni za mwenendo wa shughuli za Baraza ambazo zikitumika kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba ya 1984 zitaendelea kama ni kanuni za Baraza na amri na kanuni za mwenendo wa Baraza baada ya kuanza Katiba ya 1984, lakini zitasomwa pamoja na mabadiliko yo yote yale ambayo yatalazimika ili kuzifanya zisigongane na matakwa ya Katiba hiyo.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti na Memba wa Baraza la Mapinduzi.

9. Bila ya kuathiri masharti ya kijifungu cha (2) cha kifungu hichi na matakwa ya vifungu vilivyomo ndani ya Katiba kuhusu uchaguzi wa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na idadi ya Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, Rais wa Zanzibar na watu ambao, kabla ya kutumika kwa Katiba ya 1984 ni Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi kwa Katiba ya 1979, wataendelea kuwa Rais na Mwenyekiti na Wajumbe wa na watafanya kwa pamoja Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa Katiba mpaka hapo uchaguzi wa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi utapofanywa baada ya kutumika Katiba hiyo na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Katiba hiyo.

(2) Masharti ya kijifungu (1) cha kifungu hichi yatatumika bila kuathiri sheria yo yote ya Zanzibar inayohusu nafasi ya Rais kuwa wazi au kuondolewa kwa mtu yo yote katika wadhifa wa kuwa mjumbe wa Baraza la Mapinduzi.

Kuendelezwa kwa mashauri Mahkamani.

10. (1) Shauri lo lote ambalo limebaki katika Mahkama Kuu kabla ya kuanza kwa Katiba ya 1984, linaweza kuendelezwa na kusikilizwa, na hukumu, amri au uamuzi unaweza kutolewa na Mahkama Kuu iliyoanzishwa na Katiba hiyo.

(2) Uamuzi wo wote au hukumu au amri iliyotolewa na Mahkama Kuu iliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya 1979, au na Mahkama Kuu yo yote iliyopita na ambayo haikutekelezwa kikamilifu kabla ya kuanza kwa Katiba ya 1984 inaweza kutekelezwa baada ya kuanza kutumika kwa Katiba hiyo na Mahkama Kuu iliyoanzishwa na

Katiba hiyo na pia inaweza kutekelezwa na Mahkama za chini kwa kadri inavyowezekana na kulingana na uwezo wa Mahkama hizo.

Kufutwa kwa Katiba ya 1979 na mambo ya muda na kuhalalisha baadhi ya mambo.

11. (1) Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya 1979 inafutwa.

(2) Kitu cho chote ambacho kimefanywa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hiyo kitaendelea kutumika chini ya vifungu vya Katiba hii hadi hapo itapofutwa rasmi, au ikiwa vitendo hivyo vilikuwa kwa mujibu wa sheria iliotungwa na Baraza la Wawakilishi, hadi hapo sheria hiyo itapofutwa na kubadilishwa.

Ila tu sheria hio au kitu hicho kilichofanywa kiwe hakiendi kinyume na mataka ya Katiba hii.

(3) Amri yo yote agizo, uteuzi au kitendo chengine kilichofanywa kwa mujibu wa sheria zilizopo au sheria yo yote iliofutwa baada ya kutumika Katiba ya 1984, na ambayo sheria, hiyo ikitumika kabla ya kuanza kutumika Katiba hiyo, kitaendelea kuwa kitendo cha au amri ya halali.

Tarehe ya kutangazwa kwa Katiba.

12. Katiba ya 1979 itaendelea kufanya kazi kuanzia tarehe ambayo Katiba mpya imepitishwa na Baraza la Wawakilishi hadi siku ambayo itayokubaliwa na Rais na tarehe ya kutumika kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali la Katiba ya 1979 itasita kuwa na nguvu za kisheria mara tu baada ya Katiba mpya kuanza kutumika.

Imepitishwa katika Baraza la Wawakilishi tarehe 10 Oktoba, 1984.

[ IDI P. HASSAN ]
KATIBU
BARAZA LA WAWAKILISHI